Tahariri

## Ukarabati wa barabara Dar uharakishwe

Uk. 2

Kona ya Dkt. Bisimba

## Vijana ni nguvu ya mabadiliko leo

Safu Uk. 11

Mzee Tai

## Serikali isijifunge, itakata pumzi

Safu Uk. 5


# Pambazuko

Toleo Namba 178

Jumatatu, Agosti 17-23, 2026


## Siri kikao cha maaskofu, Rais Samia

Uk. 9

# Hospitali ya Aga Khan matatani

Uk. 6&7

- CT-Scan yalipuka mgonjwa akipimwa




# Jaji Warioba atabiri magumu

- Aingiwa wasiwasi mabadiliko ya Katiba kabla ya 2030, huku akizodoa Bunge kuwa dhaifu

Uk. 22&23



## Miaka 58 ya sauti, migongano na makali ya TEC, serikali

Uk. 12&13

Tafakuri ya Bagonza

## Huu ndiyo uanaharakati sasa

Safu Uk. 10

Tahariri

# Ukarabati wa barabara Dar uharakishwe

UJENZI na ukarabati wa barabara unaoendelea katika maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam ni uwekezaji muhimu kwa mustakabali wa maisha ya wananchi.

Barabara nzuri hupunguza gharama za usafiri, huharakisha biashara, huunganisha jamii na kurahisisha utoaji wa huduma. Zikijengwa kwa kiwango kinachostahili, zinaweza kupitika mwaka mzima bila kujali vipindi vya mvua.

Hata hivyo, faida hizo hazipaswi kutufanya tufumbe macho mbele ya madhara yanayosababishwa na miradi inayochukua muda mrefu kuliko ilivyopangwa.

Barabara inapochimbwa na kuachwa kwa miezi mingi, haiwi tena mradi wa maendeleo pekee; hugeuka kikwazo cha ustawi wa wananchi na serikali yenyewe.

Katika maeneo yenye ujenzi, wananchi hutumia muda mrefu barabarani, magari huharibika, mafuta hutumika kupita kiasi na nauli huongezeka.

Wafanyakazi hufika kazini wakiwa wamechelewa na kuchoka. Wanafunzi hukosa vipindi, wagonjwa huchelewa kufikishwa hospitalini, huku wafanyabiashara wakipoteza wateja kwa sababu maduka yao hayafikiki kwa urahisi.

Mfanyabiashara mdogo anayefungua duka kando ya barabara hawezi kuambiwa asubiri maendeleo bila kujulikana yatafika lini. Ana kodi ya pango, mishahara, leseni na familia inayomtegemea.

Vumbi likifunika bidhaa, mitaro ikaziba njia na mashine zikazuia wateja, mapato yake huporomoka. Huo ni uchumi wa kaya unaoumia kwa jina la mradi unaopaswa kuuimarisha.

Serikali pia hulipa gharama ya ucheleweshaji huo. Msongamano hupunguza uzalishaji, huongeza matumizi, huathiri ukusanyaji wa mapato na kuongeza gharama za usimamizi.

Miradi inayoongezewa muda inaweza kuhitaji fedha zaidi kutokana na kupanda kwa bei za vifaa, mabadiliko ya usanifu au kurekebisha sehemu zilizoharibika kabla hata mradi haujakamilika.

Jiji lenye watu milioni kadhaa haliwezi kuendeshwa kana kwamba muda wa wananchi hauna thamani. Kila saa inayopotea kwenye foleni ina gharama kwa uchumi, afya, familia na maisha ya wakazi wa Dar es Salaam na wageni.

Pambazuko halipingani na ujenzi wa barabara. Tunatambua kuwa ujenzi wenye ubora unahitaji muda, fedha, utaalamu na umakini, lakini muda huo lazima uwe wa kazi inayoonekana, siyo wa mitambo iliyopaki, maeneo yaliyochimbwa na kalenda inayosonga bila maelezo kwa wananchi.

Makandarasi wanapaswa kutekeleza mikataba kwa weledi, kuwa na vifaa na wafanyakazi wa kutosha, kupanga kazi kwa zamu inapowezekana na kutengeneza njia mbadala salama.

Nayo serikali kwa upande wake, ihakikishe malipo ya wajenzi yanafanyika kwa wakati, huduma kama maji na umeme zinahamishwa mapema, na usimamizi wa kila siku unaimarishwa.

Pale mkandarasi anaposhindwa bila sababu ya msingi, masharti ya mkataba yatumike. Pale taasisi ya serikali inapochelewesha uamuzi au fedha, nayo iwajibike.

Hakika siyo haki lawama zote kumwangukia mkandarasi ikiwa chanzo ni urasimu; wala siyo busara serikali kumkingia kifua mkandarasi asiye na uwezo.

Wananchi pia wanastahili taarifa za wazi kuhusu muda wa kuanza, hatua iliyofikiwa, sababu za kuchelewa na tarehe mpya ya kukamilisha mradi. Uwazi hupunguza uvumi na kuwasaidia watu kupanga shughuli zao.

Tunaihimiza serikali na makandarasi kufanya haraka kukamilisha miradi hii ya kimkakati bila kuvuruga ubora wake.

Barabara bora iliyokamilika kwa wakati ni maendeleo, lakini barabara inayojengwa bila mwisho ni jeraha linalotafuna biashara, muda, mapato na matumaini ya wananchi.

# Ni hatari kwa usalama barabarani



*Mwendesha bajaji akiwa ameijaza mizigo kuliko uwezo wake wa kubeba abiria watatu kinyume na sheria za usalama barabarani kama alivyokutwa eneo la Kimara jijini Dar es Salaam jana. (Na Mpigapich Wetu).*


## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**



## TIMU YA PAMBAZUKO

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Mhariri Mkuu** | : | Simon **MKINA** | (simon@pambazuko.or.tz) |
| **Mhariri Mtendaji** | : | Peter **NYANJE** | 0784 211 716 |
| **Mwandishi Mkuu** | : | Elizabeth **HOMBO** | 0712 792 216 |
| **Mwandishi Mwandamizi** | : | Andrew **MSECHU** | 0769 415 815 |
| **Mkuu wa DTP** | : | Yassin **LUPATU** | 0782 009 971 |
| **Mkuu wa Utawala** | : | Tryruckia **MFINANGA** | 0744 768 263 |

*Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz*

# Dunia: Hapa na Pale

## Midoli ya AI tishio jipya

TAHARUKI imeikumba Ujerumani, baada ya kuibuka kwa taarifa kuwa watu wataweza kuagiza midoli yenye akili bandia (AI) ambayo itawekwa kufanya kazi kwenye madanguro.

Midoli hiyo itachukua nafasi ya wanawake ambao wamekuwa wakifanya kazi hiyo katika maeneo ya starehe na anasa.

Wateja wataweza kukutana na kuzungumza na midoli hiyo na ”kumaliza haja zao,” hatua inayoibua mjadala mkubwa kwa watu wa Ujerumani na duniani kote.

Ripoti ya Kampuni ya Teknolojia ya SplitMetrics imebaini kuwa programu za akili bandia zimepakuliwa mara milioni 225 kwenye mtandao wa Google Play na kwamba wanaopakua, wamo wanaofanya kazi ya kuunda midoli na kuiwekea akili bandia.

## Mpango wa Iran kumuua Trump

MAMLAKA za Marekani, zimesema zimepokea onyo la tahadhari kutoka kwa vyombo vya Israel, kuwa Iran inasuka mpango wa kumuua rais wao, Donald Trump.

Mpango unaodaiwa kusukwa ili kumuua Trump umeelezwa kutumia mdunguaji aliyefuzu au kwa kutumia mshambuliaji maalumu aliyefunzwa kutumia kisu kwenye mkusanyiko wa watu wengi.

Imeelezwa kuwa mpango huo umekuwa ukiandaliwa kwa muda mrefu, tangu kumalizika kwa mashambulizi ya siku 12 ya Marekani na Israel kwa Iran mwaka 2025.



Imeelezwa mpango huo ulikuwa ni sehemu ya mkakati wa muda mrefu wa Iran kulipiza kisasi cha kuuawa kwa aliyekuwa kamanda mkuu wa kijeshi wa Iran, Qassem Soleiman mwaka 2020.

## Kenya na mkakati wa nyuklia

KENYA inajiandaa kuanza kuzalisha nishati kwa kutumia nyuklia huku kiwanda chake cha kwanza kikipangwa kuzinduliwa rasmi Machi mwaka ujao, 2027.

Kwa mara ya kwanza, mkakati huo uliwekwa hadharani na Rais William Ruto aliyetangaza kuhusu mpango huo wa nyuklia katika kongamano la kimataifa kuhusu nishati ya nyuklia lililoandaliwa jijini Nairobi, Machi 25, 2026.



Tayari maandalizi yameshika kasi, kwa ajili ya mradi huo unaokadiriwa kugharimu takriban Shilingi bilioni 500 za Kenya (karibu Shilingi trilioni tisa za Tanzania) na utazinduliwa katika Kijiji cha Lenya, Kaunti ya Siaya.

## Nyangumi asaka penzi Tanzania

WATAALAMU wa viumbe wa bahari, wameeleza kushangazwa kwao na nyangumi mwenye nundu aliyerekodiwa kutoka Colombia kwa ajili ya kutafuta majike Tanzania, ikiwa ni uhamiaji mkubwa na wa kipekee kuwahi kurekodiwa.

Wanazuoni wanaofuatilia viumbe ndani ya maji wameeleza kuwa huenda safari ya nyangumi huyo imechochewa na mabadiliko ya tabia nchi, yanayosababisha kupungua kwa hifadhi za chakula au pengine ni safari ya kutafuta wenza.

Imebainika kuwa nyangumi huyo alionekana katika Bahari ya Pasifiki karibu na Colombia mwaka 2017, kisha kuzuka tena miaka kadhaa baadaye kisiwani Zanzibar katika Bahari Hindi - umbali wa kilomita 13,000.

Ekaterina Kalashnikova anayesimamia programu ya mamalia wa baharini Tanzania amesema kwamba tukio hili ni ‘’la kushangaza na la kipekee hata kwa aina hii ya wanyama wanaohama sana.

Na Mzee TAI

# Serikali isijifunge, itakata pumzi

SERIKALI yetu siku hizi inafanana na mtu aliyefika sokoni akiwa na orodha ndefu, lakini mfukoni ana pochi nyembamba na kichwani hajui aanzie wapi.

Anataka kununua mchele, mafuta, dawa, sare za watoto na kulipa deni la jirani; mwisho wake anasimama katikati ya soko akihema, huku wauzaji wakimuuliza: “Mzee, unachukua nini?”

Hivyo ndivyo serikali ilivyo mbele ya msululu wa mambo makubwa yanayotaka uamuzi, siyo hotuba. Mezani kuna Katiba Mpya, tume mbalimbali, maridhiano ya kitaifa, majeraha ya kisiasa na ahadi ya kujenga Tanzania mpya.

Sahani imejaa mpaka punje zilizo juu zinaanza kuanguka, lakini mpishi bado anajadili kijiko gani kitumike.

Suala la Katiba Mpya limekaa sebuleni muda mrefu kiasi kwamba sasa linaweza kudai hati ya umiliki. Kila mara linaambiwa: “Subiri, wageni wataondoka.” Wageni hawaondoki; wanaongezeka. Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa 2029 unasogea, na Uchaguzi Mkuu wa 2030 nao hauko mbali.

Tukitaka sheria, taasisi na taratibu mpya zitumike kwa ufanisi, mchakato lazima uanze mapema, kwa uwazi na ushirikishwaji wa kweli.

Katiba haiandikwi kwa pupa ya dakika za majeruhi. Siyo chapati ya kugeuzwa haraka jikoni kwa sababu wateja wameanza kugonga meza.

Mimi Mzee Tai naamini kuwa tunahitaji mjadala mpana, makubaliano, sheria zinazoeleweka, elimu kwa wananchi na muda wa taasisi kujiandaa. Serikali ikichelewa, itatuambia tena muda hautoshi; kana kwamba muda huo uliibwa na wasiojulikana.

Naona pia kuna tume inayoongozwa na Jaji Shabani Ally Lila, inayochunguza makosa ya jinai yanayohusishwa na matukio ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 29, 2025 na yaliyofuata. Tume hiyo inahitaji uhuru, ushirikiano, ushahidi na majibu yanayoaminika.

Wananchi hawahitaji ripoti nyingine nzuri ya kupamba kabati. Wanahitaji ukweli, uwajibikaji na hatua zinazoonekana.

Halafu kuna maridhiano—neno tamu sana masikioni, lakini gumu sana kwa baadhi ya wanasiasa. Wanapiga danadana. Maridhiano siyo viongozi kupiga picha, kutabasamu na kunywa chai huku walioumia wakibaki nje ya ukumbi.

Ni kukubali yaliyokwenda kombo, kusikiliza maumivu, kurejesha haki, kuondoa hofu na kujenga mazingira ambayo mpinzani wa kisiasa haonekani kama adui wa taifa.

Na uzee wangu huu ninaamini kuwa Katiba Mpya itajenga uwanja sawa wa siasa, matokeo ya tume yanaweza kurejesha imani, na maridhiano yanaweza kupunguza joto la taifa.


Mambo yote haya mazito kuwa mabegani mwa serikali, naihurumia sana na kuona kana kwamba imejikaba shingo kwa kuahidi mambo mengi bila kuyawekea mpangilio unaoonekana.

Yaani naiona kabisa serikali inapumua kwa shida, siyo kwa sababu kazi haziwezekani, bali kwa sababu uamuzi unasukumwa kwa mwendo wa kobe anayesubiri kibali cha kuvuka barabara.

Ni muda muafaka sasa kwa serikali kuweka ratiba ya wazi, kutaja nani anawajibika, kutoa taarifa kwa wananchi na kutekeleza uamuzi bila hila.

Tanzania mpya haitajengwa kwa mafumbo, wala kwa kuahirisha kesho inayofika kila asubuhi. Serikali ivute pumzi, ifungue mshipi, ipange vipaumbele na ianze kazi.

Taifa haliwezi kuendelea kuhema milele likisubiri uamuzi wa kuamua lini litaamua.



Habari Kuu

# Hospitali ya Aga Khan matatani




Na Waandishi WETU

HOSPITALI ya Aga Khan ya jijini Dar es Salaam, imeingia matatani baada ya mashine yake ya uchunguzi wa kitabibu inayotumia miale ya X-ray na teknolojia ya kompyuta kutengeneza picha za ndani ya mwili wa binadamu (CT-Scan), kulipuka huku ikiwa na mgonjwa.

Taarifa za uhakika zilizolifikia Pambazuko, zimeeleza kuwa tukio hilo lilitokea Juni 4, 2026 hospitalini hapo wakati mgonjwa ambaye ni mwanafunzi wa Chuo cha Teknolojia cha Dar es Salaam (DIT), (jina tunalo), akiwa ndani ya mashine hiyo akipimwa tumbo.

Taarifa zinaeleza kuwa kijana huyo mwenye umri wa miaka 20, alifikishwa hospitalini hapo Juni 3, 2026 akikabiliwa na maumivu makali ya kichwa na tumbo yaliyoambatana na homa kali.

Baada ya uchunguzi, madaktari waliona umuhimu wa kupata uhakika wa ugonjwa unaomsumbua na ndipo wakaamua kumfanyia kipimo cha CT-Scan.

Baba mzazi wa kijana huyo, Godwin Rwakatare, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo ambapo amesema limemsababishia mwanaye tatizo la kupumua ambalo hakuwahi kuwa nalo awali.

Rwakatare amesema kutokana na kadhia hiyo ya kiafya, kijana wake ametoa jukumu la kufuatilia suala hilo kisheria na kutaka kulipwa fidia kwa kadhia hiyo iliyoteteresha afya ya kijana wake.

Mawakili kwa niaba ya mteja wao, wameandika barua kwa Hospitali ya Aga Khan kuhusu matakwa ya kisheria kulipwa fidia ya Shilingi milioni 350.

Pambazuko limeona nakala ya barua yenye Kumbukumbu Na.: AVL/BR/2026/07/14/01ya Julai 14, 2026 kutoka mawakili iliyosainiwa na wakili Makubi Kunju Makubi, ikielezea namna tukio lilivyotokea na hadi kufikia kutaka kulipwa fidia kwa mteja wao.

Barua hiyo ya mawakili inaeleza kuwa mteja wao – kutokana na kadhia hiyo, amepata maumivu ya mwili, mateso, msongo wa mawazo, matatizo ya kisaikolojia, mshtuko, usumbufu na hasara alizozipata kutokana na kile mawakili wanachoeleza kuwa ni hospitali kushindwa kutimiza wajibu wake wakati mteja wao akifanyiwa kipimo cha CT- Scan.

Barua hiyo ya wanasheria imeipa Hospitali ya Aga Khan siku 14 tangu siku ya kupokea barua hiyo kutekeleza madai yao, ikiwa ni pamoja na kuomba msamaha wa maandishi usio na utata kwa mteja wao kutokana na tukio hilo na mateso aliyoyapata.

Aidha, hospitali hiyo imetakiwa kutoa dhamana ya maandishi ya kukubali kuwajibika na kugharamia gharama zote za matibabu ya sasa na yajayo, madeni na matatizo ya kiafya yatakayothibitika kuwa yametokana moja kwa moja na tukio hilo.

“Mteja wetu alikuwa akipatiwa matibabu katika hospitali hiyo tarehe 4 Juni 2026 na kwamba alifika hospitalini hapo baada ya kusumbuliwa na maumivu ya kichwa ya muda mrefu pamoja na maumivu ya tumbo…”

Inaendelea Uk. 7

# Hospitali ya Aga...

Inatoka Uk. 6



"Tunaamini tukio hilo lilitokana na ukiukaji wa wajibu wa uangalizi wa hospitali kwa mgonjwa, kwani hospitali ina wajibu wa kisheria na kitaaluma kuhakikisha vifaa vyote vinavyotumika kwa wagonjwa vinatunzwa ipasavyo, vinapimwa mara kwa mara, ni salama na vinafaa kwa matumizi yaliyokusudiwa," inasema sehemu ya barua hiyo.

Barua hiyo inaendelea; "Pia hospitali ina wajibu wa kuhakikisha wataalamu wenye uwezo wanapatikana ili kutoa msaada wa haraka endapo dharura itatokea."

Wanasheria hao wameonya kuwa endapo hospitali hiyo itashindwa, itapuuza au kukataa kutekeleza madai hayo ndani ya muda uliowekwa, watachukua hatua za kisheria bila kutoa taarifa nyingine kwao.

Wamesema hatua hizo zitahusisha kufungua shauri la kudai fidia pamoja na gharama za kesi, riba na nafuu nyingine zote zinazopatikana kisheria.

**Danadana za Aga Khan**

Gazeti la Pambazuko limeutafuta uongozi wa hospitali hiyo kwa zaidi ya miezi miwili ili uweze kuzungumzia suala hilo, lakini liliishia kupigwa danadana.

Jumamosi - Juni 6, 2026, Pambazuko lilifika Hospitali ya Aga Khan kupata ufafanuzi wa suala hilo na mmoja wa maofisa wa hospitali hiyo aliyejitambulisha kuwa ni meneja uendeshaji, alisema taasisi hiyo kamwe haiwezi kuzungumza suala hilo kwa sababu linahusu zaidi taarifa za mgonjwa.

Ofisa huyo ambaye alijitambusha kwa jina moja la Kennedy, alisema maadili ya kitabibu hayaruhusu wao kutoa taarifa yoyote kuhusu tukio lolote la mgonjwa, ikitokea hivyo basi muhusika (mgonjwa) au ndugu zake wawe wametoa idhini hiyo, vinginevyo wao hawana ruhusa hiyo.

Ofisa huyo aliwaelekeza waandishi wa habari kwa kuwapatia simu ya ofisa mwingine wa kitengo cha biashara.

Naye alipotafutwa alisema kwamba mtu pekee anayeweza kuisemea taasisi ni mtendaji mkuu ambaye wakati huo alikuwa kwenye vikao Arusha.

Hata hivyo, aliahidi kumtafuta mtendaji na kumweleza suala hilo na angerudisha majibu kwa Pambazuko siku tatu baadaye, lakini hakufanya hivyo.

Alipotafutwa baada ya siku hizo tatu, alimshauri mwandishi kwenda moja kwa moja ofisini kwa mtendaji mkuu kuweka miadi ya kuonana naye moja kwa moja.

Pambazuko lilichukua jukumu la kuandika maswali na kuyapeleka kwa mkono ofisini kwa mtendaji mkuu wa hospitali na kuyakabidhi kwa msaidizi wake aliyejitambulisha kwa jina la Orakya Danda.

Msaidizi huyo aliahidi kufikisha ujumbe huo na akawaomba waandishi wetu kutuma maswali hayo pia kwa njia ya barua pepe ambako pia alisema majibu yangetumwa huko, jambo ambalo halikufanyika hadi leo wakati habari hii inachapishwa.

Inaendelea Uk. 8

Habari Kuu

# Hospitali ya Aga...

Inatoka Uk. 7

**Baba azungumza**

Akisimulia kisa kizima cha tukio hilo, Rwakatare anasema Juni 3, 2026 alipigiwa simu na marafiki wa mwanaye wakimjulisha kwamba hali ya kijana wake, siyo nzuri, ndipo alipokwenda kumchukua chuoni na kumpeleka Hospitali ya Aga Khan.

"Walimlaza, baada ya vipimo daktari akasema ana malaria kali, kesho yake, yaani Juni 4, 2026 tuliambiwa anapaswa kupimwa tumbo kwa mashine ya Utra sound, mgonjwa alifanyiwa maandalizi ikiwa ni pamoja na kutakiwa kunywa maji mengi…"

"Hata hivyo, nilishangaa wakati wanampeleka kwenye Utra sound walibadili mwelekeo wakaenda kwenye mashine ya CT-Scan; sikuhoji zaidi, nilijipa moyo kwamba ndivyo madaktari walivyoona inafaa…"

"Muda mfupi baada ya kipimo kuanza, mashine hiyo ilipata hitilafu ghafla na kuanza kutoa moshi mwingi wakati mtoto wangu akiwa bado ndani ya mashine, alianza kukohoa mfululizo, na asingeweza kujiokoa kwa sababu alikuwa amefungwa, hivyo kusababisha kuvuta na kumeza moshi uliosababishwa na hitilafu hiyo…"

"Waliokuwa wakimhudumia walikimbia na kumwacha ndani ya mashine, nilipiga kelele, mtoeni mwanangu anakufa... ilichukua wastani wa dakika sita kabla ya msaada kufika na kukimbizwa kitengo cha dharura na alizinduka baadaye kabla ya kupelekwa wodini," amesema.

Akiendelea kusimulia Rwakatare anasema mwanaye aliendelea kukohoa na baada ya siku moja waliruhusiwa kutoka wodini na kupangiwa siku ya kurudi tena hospitalini hapo.

Anasema kabla kuondoka alimfuata mtendaji mkuu wa hospitali hiyo na kumwuuliza kinachoendelea baada ya tukio hilo hatari kwa mwanaye. "Katika hali ambayo sikuitarajia, mkuu huyo alinijibu tu kwamba mtoto wangu amepata mshtuko tu na haoni tatizo lolote. Sikukubalina na uamuzi huo, nilimweleza suala hilo nitalifikisha kwenye vyombo vya habari na kwenye haki za kisheria," anasema Rwakatare.

> **"Waliokuwa wakimhudumia walikimbia na kumwacha ndani ya mashine, nilipiga kelele, mtoeni mwanangu anakufa...**

Mgonjwa atibiwa kwingine

Juni 11, 2026, baba wa mtoto alialikwa hospitalini hapo kwa ajili ya majadiliano kuhusu tukio hilo na uwezekano wa kulimaliza kwa njia ya mazungumzo.

Anasema katika kikao hicho ambacho pia kilihusisha wanasheria wake, hawakufikia muafaka wowote.

Hata hivyo, anasema badala ya uongozi wa hospitali kukubali kuwajibika kwa madhara yaliyotokana na tukio hilo, walipendekeza kumtibu mgonjwa kwa masharti kwamba gharama za matibabu zilipwe na mgonjwa mwenyewe.

Kutokana na hali hiyo, Rwakatare alilazimika kutafuta ushauri, vipimo na matibabu katika hospitali zingine kwa gharama zake binafsi.

Alizitaja hospitali hizo kuwa ni Amana, Apolo, Besta na Furaha zote za Dar es Salaam na kote huko wamebaini mtoto wake, amepata tatizo la kupumua kutokana na moshi.

**Ripoti ya CT-Scan yazua maswali**

Wanasheria hao pia wameibua maswali kuhusu ripoti ya CT Scan iliyotolewa na hospitali hiyo ya Aga Khan baada ya tukio hilo.

Kwa mujibu wa barua hiyo, licha ya mashine kupata hitilafu na kipimo kukatizwa, hospitali ilitoa ripoti iliyosema kuwa uchunguzi ulikuwa umekamilika na kwamba hakukuwa na tatizo lililoonekana katika eneo la tumbo.

Wanasheria hao wamesema hali hiyo inazua wasiwasi kuhusu usahihi, uaminifu na uadilifu wa ripoti hiyo ya kitabibu.

Mmoja wa wanasheria ambaye hakutaka jina lake litajwe alikiri kampuni yao kuwapelekea barua ya madai Hospitali ya Aga Khan, ambapo amesema wanamwakilisha mteja wao ambaye anaona hospitali hiyo haikutimiza majukumu yake kwa mujibu wa taaluma husika.

# Siri kikao cha maaskofu, Samia

Na Mwandishi WETU

KIKAO kilichofanywa na Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC) na Rais Samia Suluhu Hassan, Ikulu jijini Dodoma kilikuwa na usiri, nyeti na mikakati, Pambazuko limeelezwa.

Katika kikao hicho kilichofanyika Jumatatu Agosti,10, 2026, maaskofu walikwenda na hoja nzito tano kwa Rais Samia, ambazo wameshauri zifanyiwe kazi katika kuongoza juhudi zozote za kuliponya taifa.

Taarifa ya Ikulu kwa umma ilisema mazungumzo hayo yalilenga kuimarisha ushirikiano kati ya serikali na TEC pamoja na masuala mengine ya kitaifa yanayogusa jamii, yakiwamo ya kisiasa, kuimarisha amani na maendeleo, mshikamano na kujenga mustakabali mwema wa Taifa.

Chanzo cha kuaminika kimeliambia Gazeti la Pambazuko kuwa, maaskofu hao wakiongozwa na Rais wa TEC, Askofu Worfgang Pisa, walipeleka hoja tano kwa Rais Samia.

Chanzo hicho kimezitaja hoja hizo kuwa ni pamoja na kumaliziwa kwa mchakato wa Katiba mpya inayojali utu na usawa kupitia maoni ya wananchi yaliyokusanywa na Tume ya Jaji Joseph Warioba, ambapo walisisitiza uanze kwa kushirikisha wadau wote.

Maaskofu pia walihimiza kulipwa fidia kwa watu wote waliopoteza ndugu zao kwenye ghasia za Oktoba 29, 2025, na kuachiwa huru kwa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu pamoja na watu wengine walioko mahabusu kwa sababu za kisiasa.

Hoja nyingine walizomweleza Rais Samia ni kuhusu vitendo vya utekaji na kutoweka kwa watu ambapo walitaka vikomeshwe huku hoja yao ya tano ikishauri umuhimu wa kuheshimu haki za watu na kuwasikiliza.

"Katika kikao hicho hapakuwa na sauti wala vyombo vya kurekodi, maongezi yaliishia ndani, maaskofu waliwasilisha hoja zao, huku wakinukuu vifungu vya Biblia Takatifu kwa kila kipengele cha hoja walichokiwasilisha…"



*Baadhi ya viongozi wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) waliohudhulia mazungumzo na Rais Samia Suluhu Hassan, Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma karibuni. (Picha na Ikulu).*

Maaskofu pia wameshauri kuwapo maisha ya uadilifu na uwazi, ukweli na uwajibikaji ili kujenga kuaminiana.

Hoja ya matamko ya TEC mara nyingi imekuwa ikihusu kukemea ukiukwaji wa haki za binadamu, kushinikiza uwajibikaji wa serikali na kutetea ustawi wa wananchi.

Hata hivyo msimamo wao mara kwa mara umekuwa ukizua mivutano ya kisiasa na mitazamo tofauti kati ya viongozi wa dini na serikali.

### CCM yaibuka

Siku moja baada ya kikao cha Rais Samia na TEC, CCM kupitia jumuiya yake ya wazazi kimeiomba TEC kutumia nafasi yao ya dini kushawishi viongozi wa Chadema kuitikia mwito wa kurejea kwenye meza ya maridhiano ya kisiasa.

Mwito huo umetolewa Agosti 11, 2026 na Katibu wa Jumuiya ya Wazazi CCM Taifa, Ally Hapi, wakati akizungumza na wanachama wa chama hicho na wakazi wa Kilosa Mjini, mkoani Morogoro.

Hapi alipongeza hatua ya Rais Samia na Maaskofu wa Kanisa Katoliki kukutana na kujadili masuala ya kitaifa, na kusisitiza kuwa TEC imeonyesha mfano wa kuigwa wa ukomavu wa kidemokrasia unaopaswa kufuatwa na vyama vya upinzani.

Pamoja na ombi hilo la CCM, msimamo wa sasa wa Chadema kupitia viongozi wake wakuu umekuwa ukisisitiza kuwa hawatashiriki katika mchakato wowote wa maridhiano na serikali au CCM bila kuwepo kwa mpatanishi huru asiyefungamana na upande wowote.

Tafakuri ya Bagonza



Na Dkt. Benson BAGONZA

# Huu ndiyo uanaharakati sasa

NAANDIKA ili kuutetea uanaharakati. Nafanya hivi kwa sababu nimeona pande mbili zinazovutana zinaweza kusababisha tupoteze kitu muhimu sana.

Serikali yetu inawaona wanaharakati kama magaidi, lakini inatumia ugaidi kupambana na wanaharakati. Ugaidi ni mbaya bila kujali anautumia nani.

Kwa ufupi niseme, taifa letu bado linahitaji uanaharakati katika mihimili yote mitatu. Wananchi wengi ni maskini, mifumo yetu ni kandamizi, utawala wa sheria ni dhaifu; wenye elimu na nafasi wanawatumia wananchi kama vitega uchumi vyao.

Wenye fedha wa ndani na mabeberu, wanatumia wasomi na watawala kuwaumiza wananchi walio wengi. Bado tunashabikia viongozi wenye nguvu kuliko taasisi imara.

Kwa hiyo tunahitaji kuwa na mahakama ambazo zina majaji na mahakimu walio tayari kumsaidia mtu hata kama mwanasheria wao hajaomba.

Mfano, akimwona mahabusu ana majeraha amuulize kwa nini? Akiona haki yake inapotea kwa kukosea herufi, aagize irekebishwe. Akigundua mtuhumiwa amekaa polisi muda mrefu kinyume cha sheria amwachie.



Hiyo inaitwa kwa Kiingereza – Judicial Activism, yaani uanaharakati wa kimahakama. Huduma ya mahakama iwe kama hospitali. Ifanye kazi saa 24 kwa mahakimu na majaji kuingia kwa zamu.

Kwa hiyo tunahitaji bunge ambapo spika anayewaona wabunge wote ni sawa bila kujali vyama vyao. Awe jasiri asiyetishwa na chama atokacho. Mwenye upendo wa pekee kwa wabunge wanaohoji hata mamlaka ya spika kwa kutumia kanuni na katiba.

Tunahitaji spika awatie moyo wabunge kuandaa hoja binafsi na kutowapendelea wala kuwaonea mawaziri. Katiba iwe dira yake kuliko kanuni na maelekezo ya chama chake. Hiyo inaitwa Parliamentary Activism.

Na zaidi sana tunahitaji rais anayeagana na chama chake akiisha kuapishwa na kugeuka kuwa rais wa watu wote.

Tunamtaka rais "mjeuri" wa kukataa umangimeza wa kidola na itifaki zinazomtenga na hali halisi ya watu. Aliye tayari "kuasi" taratibu alizowekewa ili awahudumie watu. Anayeheshimu katiba na kutosuluhishwa na wala rushwa, wavunjaji wa haki za binadamu na awe rafiki wa wazalendo.

Tunamtaka kiongozi wa nchi anayeamini utakatifu wa Ikulu hautokani na usafi wake binafsi bali na imani yake kimatendo kwamba serikali ni mali ya wananchi.

Lazima ashtuke wananchi wasipohoji, akerwe wasipotendewa haki. Rais ambaye hata maadui zake watajiona salama mikononi mwake. Hiyo inaitwa Executive or State Activism.

Ieleweke kuwa bila uanaharakati mambo yatakuwa ni "biashara kama kawaida – kila siku, kila wakati."

Harakati za kweli zitawakatisha tamaa matapeli na watu wasio waadilifu kukimbilia siasa.

***Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.***



Na Dkt. Hellen Kijo BISIMBA

Kona ya Dkt. Bisimba

# Vijana ni nguvu ya mabadiliko leo

AGOSTI 12 ya kila mwaka dunia huadhimisha Siku ya Kimataifa ya Vijana.

Hii siyo siku ya kufanya sherehe, ni nafasi ya vijana kutafakari kuhusu nafasi yao ndani ya jamii, changamoto zinazowasonga na hata wajibu wao katika kujenga jamii wanayoitaka.

Siku hii haikutokea tu, bali ni vijana wenyewe waliliinua wazo hili mwaka 1991 walipokutana Vienna, Austria katika kikao cha kwanza cha Jukwaa la Vijana Ulimwenguni, chini ya Mfumo wa Umoja wa Mataifa.

Baada ya vijana kupendekeza uwepo wa siku yao kimataifa mwaka 1998, kongamano la mawaziri wanaohusika na vijana lililofanyika Lisbon, Ureno, walitoa pendekezo la kuwa na siku ya vijana kila Agosti 12.

Hatimaye Desemba 17, 1999, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilipitisha Azimio 54/120 kuidhinisha rasmi pendekezo hilo la mawaziri na siku hiyo ilianza rasmi 12/8/2000.

Ukitazama chimbuko hili la siku ya vijana ni ujumbe mzito kabisa kwa vijana kuwa siku hii haikutoka kwa serikali au viongozi bali ilitoka kwa vijana wenyewe na likafikia kutekelezwa.

Hii siku haipaswi kuwa siku ya watu wazima kuwaambia vijana wanachopaswa kufanya.

Hii ni siku ya vijana kuitambua sauti yao, uwezo walionao na nafasi yao katika kufanya maamuzi na hasa katika kufikia mabadiliko chanya katika jamii.

Siku hii inatukumbusha kwamba vijana ni wadau muhimu katika kujenga jamii na kwamba sauti waliyo nayo, mawazo yao na ushiriki wao katika kufanya maamuzi ni muhimu sana katika jamii zetu.

Mara nyingi tumewasikia viongozi wakisema 'vijana ni taifa la kesho'. Ukweli ni kuwa hiyo kesho huwa haifiki.

Vijana hawapaswi kusubiri kesho kwani wao wanaishi leo wakiwa na nguvu na ufahamu. Vijana hawapaswi kabisa kuwa watazamaji wa maendeleo.

Wao ni sehemu muhimu ya nguvu kazi, ubunifu, mabadiliko ya kiteknolojia, utamaduni na hata harakati za kutetea haki na uhuru wa binadamu.

Historia iko wazi kuhusu mabadiliko makubwa katika jamii yalivyohusisha vijana. Vijana wamekuwa mstari wa mbele katika kupigania uhuru, usawa, haki za binadamu na demokrasia. Hii ni kweli hata hapa nchini Tanzania.

Pamoja na kuwa vijana wa sasa wanakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo ukosefu wa ajira, fursa ndogo za kiuchumi, gharama za elimu, ukosefu wa ujuzi, kukosa nafasi za kutosha katika kufanya maamuzi, bado vijana wanapaswa kuinua sauti zao na kutafuta njia mbadala zakushikilia nafasi zao.

Vijana wawe wa kwanza kuisaidia jamii kubadili mtazamo ya kuwa vijana hawataweza kwa kukosa uzoefu.

Uzoefu wa wazee ni hazina, lakini nguvu, ubunifu na mawazo ya vijana ni mtaji wa taifa.

Pawepo na kuzungumza na kusikilizana kati ya vijana na wazee, pasiwepo na hali ya kizazi kimoja kukiona kingine kuwa mpinzani.

Vijana wanapoadhimisha siku yao watambue wana wajibu katika jamii wanapaswa kudaka fursa zitakazojitokeza na hata kuibua fursa na kuzitumia kujielimisha, kujenga ujuzi na kuitumia teknolojia kwa manufaa na zaidi kushiriki katika masuala ya jamii.

Vijana wana nafasi adhimu kulinda demokrasia, utawala wa sheria na haki za binadamu. Vijana waweze kuhoji kwa kushiriki katika mijadala ya kitaifa, kudai uwajibikaji, wainue sauti zenye hoja, maarifa na matumaini.

Vijana msisubiri kuwa viongozi wa kesho. Ninyi ni nguvu ya mabadiliko leo. Mshiriki kujenga Tanzania muitakayo leo.

***Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.***



© picture-alliance/AFP/D. Hayduk

Makala Maalum

# Miaka 58 ya sauti, migongano na makali ya TEC, serikali



*Papa John Paul II akisalimiana na Baba wa Taifa Julius Kambarage Nyerere katika ziara ya Papa nchini mwaka 1990. Kushoto kwa Mwalimu ni mkewe Mama Maria Nyerere.*

**Na Ansbert Ngurumo**

AGOSTI 10, 2026, Rais Samia Suluhu Hassan aliketi mezani Ikulu ya Chamwino, Dodoma pamoja na viongozi wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC).

Picha zikatoka. Taarifa ya Ikulu ikasema mazungumzo yalilenga kuimarisha ushirikiano kati ya serikali na TEC, kujadili masuala ya kisiasa, imani na maendeleo, na kuimarisha amani, mshikamano na mustakabali wa taifa.

Katika kikao chao, Rais Samia akawashukuru maaskofu na kuahidi kuendeleza utamaduni wa kushauriana na viongozi wa dini.

Lakini taarifa hiyo haikueleza kwa undani kwa nini maaskofu walikwenda Ikulu, wala nini hasa walimwambia Rais Samia.

Inaelezwa kuwa rais na maaskofu walikubaliana kutojadili undani wa majadiliano yao hadharani.

Watu wazima wakiaminiana kuzungumza na kushauriana juu ya mambo muhimu kwa usiri wa kimaadili na kiutawala, husimamia makubaliano yao. Ndivyo walivyofanya.

Hata hivyo, wakati hayo yakiendelea na umma ukiendelea kujadili usichojua mitandaoni na vijiweni, wakaibuka baadhi ya makada wa CCM na wanaharakati wakaanza kusimanga maaskofu wa TEC kwamba hatimaye wameufyata mbele ya serikali.

Maswali yakaibuka. Hawa wanajituma au wanatumwa? Kwanini wakubwa wao hawakemei au kuzuia kupotosha jambo lililojadiliwa kwa faragha ya utu uzima na utawala? Shabaha ya masimango haya inaponya au inaumiza taifa? Kipi kizingatiwe; propaganda au dhamiri ya mazungumzo?

Siku chache baadaye, Agosti 13, 2026, Katibu Mkuu wa TEC, Padre Dk. Charles Kitima, akatoa upande mwingine wa picha. Akaeleza vyombo vya habari kwamba maaskofu hawakuitwa Ikulu; kwamba wao ndio walioomba kukutana na Rais Samia.

Akasema walikwenda na andiko rasmi la kurasa nne, wakisisitiza umuhimu wa ukweli na msamaha katika kutafuta utulivu wa kweli wa taifa. Hapo ndipo picha ya Chamwino inapata maana kubwa zaidi.

Haikuwa picha ya Rais Samia na viongozi wa dini pekee. Ilikuwa sura mpya ya mjadala ambao Kanisa Katoliki na Serikali ya Tanzania, katika awamu hii, wamekuwa nao kwa karibu miaka sita sasa - wakati mwingine kwa maelewano, wakati mwingine kwa tahadhari, na nyakati nyingine kwa mgongano wa wazi.

Lakini uhusiano wa aina hii kati ya TEC na serikali haukuanza juzi.

Tukirudi mwaka 1968, tunagundua jambo muhimu; TEC haikuanza kama adui wa serikali. Wala historia yake haiwezi kuelezwa kwa kusema Kanisa daima limeipinga serikali.

Inaendelea Uk. 13

# Miaka 58 ya sauti...

Inatoka Uk. 12

Badala yake, historia inaonyesha TEC ikiwa taasisi ambayo mara nyingi imeunga mkono malengo ya serikali inapoona yanaendana na haki na utu wa binadamu, lakini pia imekuwa tayari kukosoa mamlaka inapohisi misingi hiyo imevunjwa.

Kwangu, hiyo ndiyo historia inayotusaidia kuielewa Chamwino ya Agosti 2026. Mkutano wa juzi kati ya rais na maaskofu, ni sehemu ya simulizi ndefu inayorudi nyuma karibu miaka sita.

Katika simulizi hilo, TEC imewahi kuipongeza serikali. Imeunga mkono sera zake. Imeshirikiana nayo katika elimu, afya na maendeleo, lakini pia imewahi kuonya, kukosoa, kuhoji mwenendo wake na, katika nyakati fulani, kutumia lugha ambayo kwa taasisi yenye hadhi na tahadhari kama Kanisa Katoliki, inaweza kuitwa kali.

Kwa hiyo, swali la msingi siyo kama TEC imewahi kuikosoa serikali. Imefanya hivyo mara nyingi.

Swali la kuvutia zaidi ni hili; Makali hayo yamekuaje kutoka awamu moja ya serikali hadi nyingine - na kwa nini? Ili kulijibu, haitoshi kuanzia kwa Rais Samia, Magufuli au hata Kikwete. Tunapaswa kurudi mwaka 1968.

Nyerere: TEC inaanza kwa kuunga mkono - lakini siyo kwa kujisalimisha

Mwaka 1967, Serikali ya Julius Nyerere ilitangaza Azimio la Arusha. Tanzania ilikuwa inatafuta mfumo wake wa maendeleo. Ujamaa na kujitegemea vikawa dira ya taifa.

Mwaka mmoja baadaye, mwaka 1968, maaskofu Katoliki wakatoa waraka muhimu; The Church and Developing Society of Tanzania.

Huu ni waraka muhimu kwa kuelewa TEC. Kwa sababu haukuanza kwa kuipiga serikali. Uliunga mkono kwa kiasi kikubwa maadili yaliyokuwa nyuma ya Azimio la Arusha; usawa, utu wa binadamu, kupunguza pengo kati ya matajiri na maskini, kupinga unyonyaji na kujenga jamii inayowajibika kwa walio dhaifu.

Kwa lugha nyingine, TEC iliona maeneo ambayo Ujamaa wa Nyerere ulikutana na mafundisho ya kijamii ya Kanisa. Hapo ndipo msingi wa uhusiano huu ulipo.

### TEC haikujijenga kama upinzani

Baraza lilijijenga kuwa sauti ya kimaadili ambayo ingeweza kusema “ndiyo” pale serikali ilipoonekana kwenda katika mwelekeo sahihi, au “hapana” pale mbinu au matokeo yalipoonekana kukiuka misingi iliyokuwa imeungwa mkono.

Na haikuchukua muda kabla sehemu ya pili haijaanza kuonekana. Kadiri sera za Ujamaa zilivyotekelezwa, hususan vijijini, umiliki wa mali, shughuli za taasisi binafsi na nafasi ya dola katika maisha ya wananchi, baadhi ya viongozi wa kanisa wakaanza kuonyesha wasiwasi.

Hapa ndipo tofauti kati ya lengo na njia ilipojitokeza. Kanisa lingeweza kuunga mkono usawa, lakini likauliza; usawa unaletwa kwa njia gani? Lingeweza kuunga mkono maendeleo ya vijijini lakini likauliza; wananchi wanashirikishwa kwa kiwango gani? Lingeweza kukubali wajibu wa serikali katika kujenga taifa, lakini likauliza; mamlaka ya serikali yanaishia wapi?

Mvutano huo ulikuwa mkubwa kiasi kwamba Agosti 3, 1970, Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere alizungumza na Katibu Mkuu wa TEC wa wakati huo, Padre Robert Rweyemamu, kuhusu shaka iliyokuwa ikitolewa na baadhi ya viongozi wa kanisa kuhusu Ujamaa.

Inaendelea Uk. 14



*Papa John Paul II alipotembelea Tanzania kwa mwaliko wa Rais Ali Hassan Mwinyi kuanzia Septemba 1 hadi 10 Septemba 1990.*

Makala Maalum

# Miaka 58 ya sauti...

Inatoka Uk. 13

Hii ni hatua muhimu sana katika historia yetu. Kwa sababu miaka miwili tu baada ya TEC kuunga mkono misingi ya Azimio la Arusha, tayari kulikuwa na tofauti kuhusu utekelezaji wake.

Hapo ndipo tunapata jambo muhimu zaidi kuhusu uhusiano ambao utaendelea kwa miongo kadhaa, yaani ushirikiano bila kujisalimisha.

1970 na kuendelea: Kanisa linaanza kuuliza gharama ya sera

Katika miaka iliyofuata, masuala ya utaifishaji, elimu, huduma za jamii, vijiji vya ujamaa na nafasi ya taasisi za dini, yaliendelea kuleta mijadala. Kanisa Katoliki lilikuwa limewekeza sana katika shule na hospitali. Serikali nayo ilikuwa inapanua wajibu wake katika maeneo hayo.

Hivyo, mjadala haukuwa wa kinadharia. Uligusa mali, taasisi, walimu, wagonjwa, wanafunzi na nafasi halisi ya kanisa katika jamii.

Makali ya TEC ya wakati huu hayakuwa sawa na yale tutakayoyaona mwaka 2018 au 2025. Lugha ilikuwa zaidi ya ushauri, tahadhari na mafundisho ya kijamii kuliko "mapambano" ya moja kwa moja.



*Rais Benjamin Mkapa akiwa katika picha ya pamoja na Maaskofu wa Kanisa Katoliki (TEC).*

Lakini mbegu ilikuwa tayari imepandwa - kwamba serikali haiwezi kuwa ndiyo mamlaka pekee ya kuamua kilicho chema kwa jamii.

Mwinyi: TEC inaanza kuzungumza zaidi kuhusu serikali yenyewe

Rais Ali Hassan Mwinyi alipoingia Ikulu mwaka 1985, Tanzania ilikuwa tofauti.

Ujamaa ulikuwa unapoteza nguvu yake ya kiuchumi. Uchumi ukaanza kufunguliwa. Masharti ya taasisi za fedha za kimataifa yakaingia. Baadaye mfumo wa chama kimoja ukaondoka na vyama vingi vikarejea mwaka 1992.

Lakini pamoja na uhuru zaidi wa kiuchumi na kisiasa, matatizo mengine yakawa yanaonekana; rushwa, pengo la matajiri na maskini, maadili ya viongozi kuporomoka, migogoro ya kidini, suala la Zanzibar na swali la namna Tanzania mpya ya vyama vingi ingeongozwa.

Hapa TEC ikaanza kupanua lugha yake.

1992: True Human Development

Mwaka 1992 maaskofu walitoa waraka uliopewa jina la True Human Development.

Hapa TEC ilikuwa inarudisha hoja ya maendeleo kwenye msingi mmoja muhimu; maendeleo siyo takwimu za uchumi peke yake.

Maendeleo lazima yamhusu binadamu, utu wake, uhuru wake, haki yake, mahitaji yake ya msingi, pia uwezo wake wa kushiriki katika uamuzi unaohusu maisha yake.

Ni muhimu kwamba waraka huu ulitokea wakati Tanzania ilikuwa inabadilika kutoka mfumo wa chama kimoja kwenda vyama vingi.

Kwa hiyo TEC ilikuwa, kwa namna yake, ikiweka kipimo cha kimaadili juu ya Tanzania iliyokuwa inazaliwa upya kisiasa.

**1993 - 1994: Dini, Zanzibar na serikali**

Kisha mjadala ukawa mkali zaidi. Mwanzoni mwa miaka ya 1990, Tanzania ilikumbwa na mvutano wa kidini.

Kulikuwa na malalamiko ya viongozi wa Kikristo kuhusu mahubiri na vitendo vilivyoonekana kudhalilisha Ukristo. Kulikuwa pia na mjadala mkubwa kuhusu Zanzibar na Organization of Islamic Conference (OIC).

Inaendelea Uk. 15

# Miaka 58 ya sauti...

Inatoka Uk. 14

TEC na taasisi nyingine za Kikristo, zikaonyesha wasiwasi. Serikali ya Mwinyi ikajikuta katikati ya mjadala wenye hatari kubwa; dini, Muungano na siasa.

Rais Mwinyi akakutana na viongozi wa Kikristo.

Hapa tunaona mwelekeo ambao utarudi tena miaka mingi baadaye ambapo Kanisa linatoa malalamiko hadharani, hali ya kisiasa inakuwa tete, Ikulu inaingia, viongozi wanakutana.

Lakini kipindi cha Rais Mwinyi kinaonyesha pia ongezeko la makali ya TEC. Sasa haizungumzi tu kuhusu falsafa ya maendeleo. Inazungumzia mwenendo wa serikali, ulinzi wa haki, rushwa, dini na uadilifu wa mamlaka.

Mkapa: Kutoka maadili hadi uwajibikaji wa dola

Rais Benjamin Mkapa alipoingia madarakani mwaka 1995, rushwa ilikuwa mojawapo ya matatizo makubwa yaliyokuwa yakizungumzwa nchini.

Mkapa mwenyewe alikiri tatizo hilo na kuunda Tume ya Jaji Joseph Warioba kuchunguza mianya ya rushwa. Kwa TEC, hili lilikuwa suala la kimaadili.

Katika kipindi hiki, ujumbe wa Kanisa uliendelea kusisitiza uongozi wa maadili, matumizi ya haki ya rasilimali, kupunguza umaskini, wajibu wa viongozi na haki za wananchi.

Lakini jambo jingine lilikuwa linatokea. Mageuzi ya kiuchumi yalikuwa yanaanza kubadilisha Tanzania.

Mashirika ya umma yalibinafsishwa. Sekta ya madini ilipanuka. Wawekezaji wa nje wakaongezeka, lakini wananchi wengi waliendelea kuwa maskini.

Hapo Kanisa likauliza swali ambalo litaendelea kulirudia katika awamu zinazofuata; Maendeleo haya ni kwa ajili ya nani?

Hili ndilo daraja kati ya TEC ya Nyerere na TEC tutakayoiona baadaye katika mjadala wa rasilimali, Bandari. Hoja yake ya msingi haikubadilika sana. Kilichobadilika ni mazingira.

### Uchaguzi na dhamiri ya mpiga kura

Katika kipindi cha mfumo wa vyama vingi, TEC pia ilianza kutoa mwongozo wa mara kwa mara kuelekea uchaguzi.



*Rais mstaafu Jakaya Kikwete akiwa katika picha ya pamoja na Maaskofu wa Kanisa Katoliki (TEC).*

Maaskofu walihimiza waamini na wananchi kupiga kura kwa dhamiri, kuchunguza tabia na uwezo wa wagombea na kutokubali rushwa ya uchaguzi.

Hili linaweza kuonekana jambo la kawaida leo, lakini lina maana kubwa. Kwa kufanya hivyo, Kanisa lilikuwa limekubali kwamba ubora wa uongozi wa kisiasa ni suala la kimaadili.

Hapo ndipo mlango ulifunguliwa zaidi. Kwa sababu ukishasema wananchi wachague viongozi waadilifu, lazima uwe tayari pia kusema nini kinatokea viongozi wanapokosa uadilifu.

Kikwete: TEC inakaribia zaidi kiini cha mamlaka

Rais Jakaya Kikwete aliingia madarakani mwaka 2005 akiwa na umaarufu mkubwa, lakini kadiri miaka ilivyopita, mijadala kuhusu rushwa, ufisadi, rasilimali, uwajibikaji na Katiba ikawa mikubwa. TEC nayo ikawa sehemu ya mijadala hiyo.

### EPA, Richmond na maadili ya uongozi

Kipindi cha Kikwete kilikumbwa na kashfa kubwa zilizotikisa serikali. Richmond ilisababisha Waziri Mkuu Edward Lowassa kujiuzulu mwaka 2008. EPA ikawa mjadala mkubwa wa fedha za umma.

Inaendelea Uk. 16



# Miaka 58 ya sauti...

Inatoka Uk. 15

Kanisa na viongozi mbalimbali wa dini wakazidi kusisitiza uwajibikaji, kupinga rushwa na kulinda mali ya umma.

Hapa makali ya TEC yalikuwa yanaingia hatua nyingine. Haikutosha tena kusema: "Viongozi wawe waadilifu."

Sasa mazingira yalikuwa yanailazimisha jamii kuuliza; "Kiongozi asipokuwa mwadilifu, nani anamwajibisha?"

**2010: TEC na uchaguzi**

Katika maandalizi ya uchaguzi wa 2010, TEC ilitoa mwongozo uliosisitiza wajibu wa wananchi kuchagua viongozi wenye uwezo, uadilifu na kujali maslahi ya Taifa. Waraka huo ulizua mjadala mkubwa wa kisiasa.

Baadhi ya watu waliona Kanisa linaelimisha wapiga kura. Wengine wakahisi lugha yake ingeweza kutafsiriwa kama "kuelekeza uchaguzi."

Hapa ndipo tatizo ambalo TEC itaendelea kukabiliana nalo linapoonekana wazi, kwamba unawezaje kutoa mwongozo wa kimaadili kuhusu uchaguzi bila kuonekana unachagua upande wa kisiasa?

**2014–2015: Katiba Mpya**

Lakini moja ya hatua muhimu zaidi za TEC katika awamu ya Kikwete ilikuwa Katiba. Mchakato wa Katiba Mpya ulianza kwa matumaini makubwa.

Tume ya Jaji Joseph Warioba ikakusanya maoni ya wananchi. Rasimu ikatolewa. Bunge Maalumu la Katiba likaingia. Mgogoro ukazuka.

Mwaka 2015, maaskofu Katoliki wakatoa waraka uliosainiwa na maaskofu 34. Walikuwa na shaka kubwa kuhusu mchakato ulivyokwenda. Walizungumza kuhusu uadilifu wa mchakato, ushirikishwaji na namna maoni ya wananchi yalivyoshughulikiwa.

Hili lilikuwa jambo kubwa. TEC haikuwa tena inazungumza pembeni ya mfumo. Ilikuwa inazungumza kuhusu sheria mama inayounda mfumo wenyewe.

Makali yalikuwa yameongezeka - kutoka "Ujamaa utekelezwe kwa haki" kwenda "viongozi wawe waadilifu;" hadi "wananchi wachague kwa dhamiri."

Na sasa imekuwa "mchakato unaounda Katiba yenyewe lazima uwe wa haki na uaminifu."

Magufuli: TEC inataja dalili za kuvunjika kwa demokrasia

Rais John Magufuli alipoingia madarakani mwaka 2015, alianza kwa nguvu kubwa ya kisiasa.

Kwa wengi wasiojua mambo ya ndani ya serikali, alionekana anapambana na ubadhirifu. Alifukuza watumishi. Alitembelea taasisi kwa kushtukiza.

Akasisitiza nidhamu na ukusanyaji wa mapato. Wananchi wengi wakampokea kama "rais wa vitendo." Lakini kadiri muda ulivyopita, sura nyingine ya Magufuli ilianza kujitokeza. Mikutano ya kisiasa - hasa ya wapinzani - ikabanwa. Vyombo vya habari vikakabiliwa na shinikizo - vikatishwa na kufungiwa.

Wanasiasa na wanaharakati wakosoaji wakakamatwa. Baadhi ya watu wakashambuliwa, wakatekwa, wapotea au wakauawa. Hapa TEC ikabadilisha sauti.

**Waraka wa Kwaresima wa 2018**

Hili ni mojawapo ya matamko muhimu zaidi katika historia ya TEC baada ya mfumo wa vyama vingi. Maaskofu wote 36 waliweka majina yao katika waraka uliogusa hali ya kisiasa nchini.

Walizungumzia hofu. Walizungumzia uhuru wa kujieleza. Walizungumzia uhuru wa vyombo vya habari. Walizungumzia mazingira ya vyama vya siasa.

Walizungumzia watu waliokuwa wakipotea au kushambuliwa. Walizungumzia haki na wajibu wa serikali kulinda wananchi. Hapa lugha ya TEC ilikuwa imeendambali sana na 1968.

Mwaka 1968, kanisa lilikuwa likizungumza kuhusu namna ya kujenga jamii ya ujamaa yenye haki. Mwaka 2018 lilikuwa linauliza kama mfumo wa kisiasa wenyewe ulikuwa unaheshimu haki za msingi za wananchi.

Inaendelea Uk. 17

# Miaka 58 ya sauti...

Inatoka Uk. 16

Haya ndiyo “makali ya TEC” tunayotafuta katika historia hii. Hayakutokea ghafla. Yalikua hatua kwa hatua.

### Serikali yajibu

Waraka huo haukupokelewa bila msuguano. Kulikuwa na mjadala mkali kuhusu kama viongozi wa dini walikuwa wamevuka mpaka na kuingia katika siasa.

Barua iliyodaiwa kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani kuhusu TEC na KKKT ilisambaa na kuzua taharuki, ingawa serikali baadaye iliikana.

Lakini jambo kubwa zaidi lilikuwa tayari limetokea; TEC ilikuwa imeweka hadharani wasiwasi ambao ulikuwa unasikika sehemu nyingine za jamii. Na serikali ilikuwa imelazimika kujibu.

Ni katikati ya mvutano huu, Katibu Mkuu wa TEC, Padre Raymond Saba, alivuliwa uraia, akanyang’anywa pasipoti. Ndipo TEC Ikamteua Dkt. Charles Kitima. Baadaye Padri Saba akafariki dunia katika mazingira yenye utata.

### 2020: Uchaguzi Mkuu unaongeza makali

Kadiri uchaguzi mkuu wa 2020 ulivyokaribia, maswali kuhusu mazingira ya kisiasa yaliongezeka. Viongozi wa dini wakasisitiza amani, haki, uchaguzi wa kuaminika na wajibu wa taasisi za uchaguzi.

Baada ya uchaguzi, kulikuwa na malalamiko makubwa kutoka upinzani na mashirika mbalimbali kuhusu mchakato. Wakasema uchaguzi haukufanyika. Wakauita “uchafuzi.”

Hapa pia Kanisa lilikuwa katika mazingira magumu. Lilitakiwa kuhubiri amani. Lakini amani yenyewe ilikuwa inahitaji haki.

Hili ndilo jambo ambalo baadaye litakuwa muhimu sana katika lugha ya TEC chini ya Samia, kwamba “amani siyo ukimya” na kwamba msingi wa amani ni haki. Samia: Kutoka maridhiano hadi uchaguzi na Oktoba 29

Rais Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani Machi 2021, alirithi nchi iliyokuwa na migawanyiko mikubwa ya kisiasa. Tanzania ilijawa na hofu kila mahali.

Hatua zake za mwanzo zilitoa matumaini. Mazungumzo yakaanza. Baadhi ya vizuizi vikalegezwa. Mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa baadaye ikaruhusiwa.



*Rais Dkt. John Pombe Magufuli akiwa katika mazungumzo na Rais wa Baraza la Maaskofu wa Kanisa Katoliki (TEC) Askofu Gervas John Nyaisonga, Makamu wa Rais wa Baraza lhilo Dkt. Flavian Kasalla wakiwa na Katibu Mkuu wa TEC Dkt. Charles Kitima, Ikulu jijini Dar es salaam Agosti 7, 2018*

Neno maridhiano likawa sehemu ya lugha ya kisiasa ya Taifa. Wananchi wakampa rais jina jipya - “mama.”

Lakini TEC haikuacha jukumu lake la kukosoa.

Mwaka 2023, mjadala kuhusu makubaliano ya Tanzania na Dubai kuhusu bandari ulilipuka. Kelele zikapigwa kila kona. TEC ikaingia moja kwa moja.

Maaskofu walitaka serikali kusikiliza zaidi wananchi na wakatoa tahadhari kuhusu makubaliano hayo ya DP World.

Hii ilikuwa hatua kubwa kwa sababu bandari siyo suala la ibada. Ni uchumi. Ni uwekezaji.Ni mamlaka ya Serikali. Ni mikataba ya kimataifa. Ni rasilimali ya Taifa.

Kwa wakosoaji wa TEC, hapa Kanisa lilikuwa limeingia katika eneo ambalo lilipaswa kuachiwa serikali na wataalamu.

Lakini kwa TEC, suala lilikuwa na “dimension” nyingine; kwamba mali ya taifa inasimamiwaje kwa maslahi ya wananchi?

Ukirudi nyuma hadi kipindi cha Mkapa na mijadala kuhusu rasilimali, utaona mwendelezo. TEC ilikuwa inapanua matumizi ya mafundisho yake ya kijamii hadi kwenye usimamizi wa mali ya umma.

2024 - 2025: Lugha inakuwa nzito zaidi

Inaendelea Uk. 18

## Makala Maalum



# Miaka 58 ya sauti...

Inatoka Uk. 17

Kadiri mazingira ya uchaguzi mkuu wa 2025 yalivyoanza kujengwa, TEC ilizidi kuzungumzia haki, amani na mazingira ya kisiasa.

Hapa ndipo tunafikia hatua ambayo "makali" yake hayawezi tena kupimwa kwa waraka mmoja. Ni mlolongo. Matamko. Mahubiri. Tahadhari.Sala. Wito wa mazungumzo. Na kisha matukio halisi.

Aprili 30, 2025, Katibu Mkuu wa TEC, Padri Charles Kitima, akavamiwa na kushambuliwa katika makao makuu ya TEC Kurasini.

Tukio hilo lilikuwa na uzito mkubwa kwa sababu sasa mtu aliyekuwa mmoja wa sauti zinazotambulika zaidi za kanisa katika masuala ya taifa alikuwa ndiye mwathirika wa shambulio.

TEC ikataka uchunguzi. Na baadaye ikaonyesha kutoridhishwa na kasi ya uchunguzi huo.

Juni 2025: Sala na kufunga kwa ajili ya taifa

TEC ikaitisha sala na kufunga kwa ajili ya haki na amani kuelekea uchaguzi.

Kwa nje hili linaweza kuonekana jambo la kidini kabisa, lakini katika muktadha wa wakati huo, ujumbe wake ulikuwa mzito.

Kanisa lilikuwa linasema taifa lina tatizo ambalo haliwezi kutatuliwa kwa taratibu za uchaguzi pekee. Linahitaji haki. Linahitaji ukweli. Linahitaji dhamiri.

Oktoba 29, 2025: mstari unakatika

Kisha ukaja uchaguzi mkuu. Na vurugu. Na vifo. Hapa ndipo historia ya matamko ya TEC inapofikia kilele chake.

Baada ya matukio ya Oktoba 29 na yaliyofuata, TEC haikutoa tu wito wa kawaida wa amani. Maaskofu walitaka uchunguzi huru.

Walizungumza kuhusu mauaji. Walitaka waliofungwa katika mazingira ya uchaguzi waachiwe. Walitaka haki. Walirudisha hoja ya Katiba Mpya.

Hii ilikuwa tofauti muhimu katika harakati na mchakato mzima.

Katika historia ya TEC, tumetoka mwaka 1968 ambapo maaskofu walikuwa wanajadili namna Ujamaa unavyoweza kujenga jamii ya haki. Sasa, mwaka 2025, maaskofu walikuwa wanauliza Serikali kuhusu damu ya wananchi.

Huwezi kuelewa makali ya tamko hili bila kuona safari nzima. 1968: maendeleo yenye haki. 1992: maendeleo yanayomheshimu binadamu. Miaka ya 1990: rushwa, dini na haki. Miaka ya Mkapa: maadili, umaskini na uwajibikaji. 2010: dhamiri ya mpiga kura. 2015: uadilifu wa mchakato wa Katiba. 2018: demokrasia, hofu, uhuru na watu kupotea. 2023: rasilimali na DP World. 2025: uchaguzi, vurugu, vifo na uchunguzi huru.

Huo ndio mstari wa makali ya TEC.

2026: Kutoka tamko hadi mezani

Mwaka 2026, TEC haikufunga mjadala. Katika Mkutano Mkuu wake wa 87, maaskofu walirudia hoja za haki, rasilimali, mazungumzo na uponyaji wa Taifa.

Halafu wakafanya jambo muhimu. Wakaomba kumuona Rais. Agosti 10, wakaenda Chamwino. Ikulu ikatoa picha na taarifa.

Lakini siku chache baadaye Padri Charles Kitima akaeleza jambo ambalo linabadilisha namna ya kuutafsiri mkutano ule: Maaskofu hawakuitwa. Wao ndio walioomba kukutana na Rais.

Na hawakwenda mikono mitupu. Walikuwa na andiko lao. Kwa hiyo picha ya Chamwino haikuwa mwisho wa matamko ya TEC. Ilikuwa mwendelezo wake kwa njia nyingine.

Baada ya kusema hadharani, kanisa lilikwenda kusema moja kwa moja kwa mwenye mamlaka.

Je, TEC imekuwa kali zaidi?

Ukiangalia miaka 58 kwa pamoja, jibu ni ndiyo - lakini linahitaji maelezo.

Siyo kwamba maaskofu wa leo wana hasira zaidi kuliko wa 1968. Ni kwamba masuala wanayokabiliana nayo yamebadilika.

Inaendelea Uk. 19

# Miaka 58 ya sauti...

Inatoka Uk. 18

Nyerere alikuwa anajenga mfumo mpya wa maendeleo. Mwinyi alikuwa anafungua uchumi na mfumo wa kisiasa.

Mkapa alikuwa anakabiliana na rushwa na mageuzi ya uchumi. Kikwete alikabili mjadala wa Katiba na uwajibikaji.

Magufuli alikabili maswali kuhusu uhuru wa kisiasa na haki za kiraia. Samia anakabili urithi wa masuala hayo yote pamoja na jeraha la uchaguzi wa 2025.

Kwa hiyo lugha ya Kanisa imekuwa kali kadiri mada yenyewe ilivyokuwa nzito. Ni tofauti kuzungumzia sera ya maendeleo na kuzungumzia kifo cha mwananchi.

**Lakini TEC siyo serikali mbadala**

Hapa lazima kuwe na tahadhari. Historia hii isitufanye tuiweke TEC juu ya ukosoaji.

Kanisa nalo linaweza kukosea katika tathmini yake ya kisiasa. Linaweza kukosa taarifa ambazo serikali inazo, lakini matamko yake yanapimwa katika dhamira ya kanisa kwenye muktadha wa utume wa maaskofu. Yanabeba sauti ya ufalme, ukuhani, na unabii.

Baadhi ya kauli zake zinaweza kutafsiriwa na wananchi kwa maana tofauti. Na ikumbukwe kuwa Wakatoliki wenyewe hawana msimamo mmoja wa kisiasa.

TEC siyo Bunge. Siyo mahakama. Siyo chama cha siasa. Na haiwezi kuchukua nafasi ya taasisi hizo.

Lakini pia siyo sahihi kusema; "Viongozi wa dini wabaki madhabahuni." Kwa sababu historia yenyewe inakataa hoja hiyo.

Kanisa limekuwa mshirika wa serikali katika elimu, afya na maendeleo kwa miongo mingi. Kama lina wajibu kwa ustawi wa mwili wa mwananchi hospitalini, linawezaje kukosa wajibu wowote kwa utu wake anapodhulumiwa?

Hapo ndipo msingi wa hoja ya TEC ulipo.

Serikali nayo ina hoja

Serikali ina wajibu wa kulinda taifa lisigawanywe kwa misingi ya dini. Ina haki ya kutaka viongozi wa dini wasigeuze madhabahu kuwa majukwaa ya kampeni.

Ina haki ya kujibu hoja ambazo inaamini hazina taarifa kamili. Na haiwezi kutekeleza kila pendekezo la maaskofu kwa sababu tu limetolewa na kanisa.

Lakini mamlaka yenye nguvu haihitaji ukimya wa wakosoaji wake ili ithibitishe nguvu yake. Inaweza kusikiliza. Inaweza kujibu. Inaweza kukataa. Inaweza kurekebisha.

Huo ndio ukomavu wa taasisi.

Ndiyo maana Chamwino ni muhimu

Mkutano wa Agosti 10, 2026 una maana kubwa zaidi ukiwekwa mwisho wa mfululizo huu wa hatua za maaskofu

Inaendelea Uk. 20



*Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na viongozi wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma karibuni. (Picha na Ikulu).*

■ Makala Maalum

# Miaka 58 ya sauti...

Inatoka Uk. 19

TEC haikufika Chamwino kutoka ombwe. Ilibeba historia. Ilibeba 1968. Ilibeba mijadala ya Ujamaa. Ilibeba miaka ya Mwinyi.

Ilibeba maadili na uwajibikaji wa miaka ya Mkapa. Ilibeba Katiba ya Kikwete. Ilibeba waraka wa 2018. Ilibeba DP World.

Ilibeba kifo cha Padri Saba. Ilibeba shambulio la Padri Kitima. Na zaidi ya yote, ilibeba Oktoba 29 - uchaguzi wenye utata na vifo vya raia.

Kwa hiyo, swali baada ya mkutano wa juzi Ikulu si kama rais na maaskofu walitabasamu.

Swali ni: Nini kitabadilika? Je, kutakuwa na ukweli kuhusu yaliyotokea? Je, kutakuwa na uwajibikaji? Je, waliofiwa watapata majibu?

Je, uchunguzi utakuwa na kiwango cha uhuru kinachoweza kujenga imani? Je, waliojeruhiwa kisiasa na kijamii watasikilizwa?

Je, Katiba Mpya itarudi mezani? Je, Serikali itayaona maridhiano kama mchakato wa kubadilisha mazingira au kama mkutano wa viongozi?

Na TEC yenyewe itafanya nini kama mambo ambayo iliwasilisha kwa Rais Samia hayatatekelezwa? Hapo ndipo hatua inayofuata ya historia hii ilipo.

Miaka 58 ya kusema ukweli mbele ya mamlaka

Ukiweka matamko haya pamoja, jambo moja linaonekana.

Makali ya TEC hayakuzaliwa mwaka 2025. Hayakuanza na Samia. Hayakuanza na Magufuli. Wala hayakuanza na DP World.

Yamejengwa polepole katika historia ya taifa. TEC ya 1968 ilisema maendeleo lazima yawe ya haki. TEC ya miaka ya Mwinyi ikasema maendeleo lazima yamheshimu binadamu na Serikali iwajibike katika mazingira mapya.

TEC ya Mkapa ikaendelea kuunganisha uongozi na maadili, umaskini, rushwa na matumizi ya rasilimali. TEC ya Kikwete ikaingia hadi katika uadilifu wa uchaguzi na Katiba.

TEC ya Magufuli ikasema wazi kwamba uhuru, demokrasia na usalama wa wananchi viko ndani ya eneo la dhamiri ya Kanisa.

TEC ya Samia ikaenda hatua nyingine: rasilimali za taifa, uchaguzi, mauaji, uchunguzi huru, Katiba, ukweli na maridhiano.

Huu si mstari ulionyooka.

Wakati mwingine TEC imekuwa kimya, wakati wananchi wengine wakitaka izungumze. Wakati mwingine imezungumza, na baadhi ya watu wakaona imechelewa.

Wakati mwingine imeonekana ipo karibu sana na Serikali. Wakati mwingine imeonekana mbali sana nayo.

Hilo lenyewe linastahili uchambuzi. Lakini katika miaka 58, msingi mmoja umeendelea kujitokeza: TEC imekataa kukubali kwamba utii kwa mamlaka unamaanisha ukimya mbele ya mamlaka.

Na Serikali zote, kuanzia Nyerere hadi Samia, kwa namna tofauti, zimelazimika kuishi na ukweli huo.

Kwangu, hiyo ndiyo maana kubwa ya picha za Chamwino. Si picha za serikali na kanisa ambazo ghafla zimeamua kuwa marafiki.

Ni picha za taasisi mbili ambazo zimekuwa zikishirikiana, zikivutana, zikikosana, zikijibu, zikionya na kurudi mezani kwa zaidi ya nusu karne.

Na pengine hapo ndipo Tanzania inaweza kupata somo kubwa zaidi. Taifa lenye afya halihitaji kanisa linaloogopa serikali. Wala halihitaji kanisa linalotaka kuwa serikali.

Linahitaji taasisi yenye uwezo wa kusema: "Hapa tumekubaliana nanyi." Na inapobidi: "Hapa hatukubaliani nanyi."

Serikali yenye afya nayo haihitaji kuona kila anayeikosoa ni adui. Inahitaji uwezo wa kusikiliza bila kupoteza mamlaka, kujibu bila kutisha na kurekebisha inapobidi bila kuona marekebisho kama udhaifu.

Mwaka 1968, TEC iliingia katika mjadala kuhusu Tanzania iliyokuwa inajengwa. Agosti 10, 2026, ikaingia Ikulu kujadili Tanzania iliyojeruhiwa na namna ya kuijenga tena.

Kati ya matukio hayo mawili kuna miaka 58 ya historia. Na ukifuatilia matamko yake moja baada ya jingine, unaona kitu ambacho picha moja ya Chamwino haiwezi kuonyesha:

Kadiri maswali ya Taifa yalivyokuwa mazito, ndivyo sauti ya TEC ilivyozidi kuwa kali.

Sasa swali siyo kama TEC itasema nini tena, swali kubwa zaidi ni kama, baada ya miaka 58 ya kusema, mamlaka itasikia nini.

***Mwandishi wa makala haya maalum ni mwandishi, mchambuzi wa siasa, mwalimu na muumini wa Kanisa Katoliki. Imechapwa baada ya kuhaririwa kuendana na staili ya Pambazuko.***

# Samia kuzindua JNHPP Agosti 22

Na Mwandishi WETU



RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuzindua rasmi Kituo cha Kuzalisha Umeme cha Julius Nyerere (JNHPP) chenye uwezo wa kuzalisha megawati 2,115.

Akizungumza na waandishi habari juzi jijini Dar es Salaam, Waziri wa Nishati, Deogratius Ndejembi amesema mkuu huyo wa nchi atazindua kituo hicho Agosti 22, 2026 katika eneo la mradi lililopo Rufiji, Mkoa wa Pwani. Pamoja na mambo Ndejembi amesema uzinduzi huo pia utahudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, wageni kutoka ndani na nje ya nchi, wananchi na wadau wa maendeleo. "Uzinduzi huu wa mradi wa umeme wa Julius Nyerere ni tukio la kihistoria na hatua muhimu katika safari ya Tanzania ya kujenga mfumo wa nishati ya uhakika nchini, sambamba na kuchochea shughuli za uzalishaji, uwekezaji na ukuaji wa uchumi…"

"Huu ni mradi mkubwa zaidi wa kuzalisha umeme kuwahi kutekelezwa nchini kwa kutumia fedha za ndani za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ukiwa na uwekezaji wa takribani Shilingi trilioni 7.452,"amesema Ndejembi. Akifafanua kuhusu mradi huo, amesema JNHPP imeendelea kuongeza kiwango cha umeme kinachoingia katika Gridi ya Taifa na hivyo kusaidia kupunguza changamoto za upungufu wa uzalishaji zilizokuwa zikichangia mgao wa umeme nchini.

Ndejembi amesema hadi Mei 31, 2026, kituo hicho kilikuwa kimezalisha takribani asilimia 44.9 ya umeme wote uliozalishwa na kuingia katika Gridi ya Taifa katika kipindi cha mwaka mmoja. "Hivyo kituo hicho kimekuwa kikichangia takribani nusu ya umeme wote unaotumika nchini Tanzania,"amesema waziri Ndejembi.

Waziri huyo amesema kuwa kwa sasa uwezo wa mitambo yote ya kuzalisha umeme nchini umefikia takribani megawati 4,648.

"Hivyo ongezeko la megawati 2,115 itakuwa ni kiwango kikubwa wa taifa kukidhi mahitaji ya umeme na kuimarisha usalama wa nishati,"amesema.

Ndejembi amesema mbali na uzalishaji wa umeme, mradi huo una uwezo wa kuchangia katika udhibiti wa mafuriko katika Bonde la Rufiji, kilimo cha umwagiliaji, utalii na upatikanaji wa maji kwa matumizi mbalimbali.

Aidha ametaja mradi wa kusafirisha umeme wa megwati 400 kutoka Chalinze kwenda Dodoma kuwa miongoni mwa miradi inayotekelezwa kuimarisha uwezo wa kusafirisha umeme.

Ujenzi wa mradi huo ulianza Juni 2019 na kukamilika Machi 2025.

Katika kipindi cha ujenzi huo takribani wafanyakazi 12,000 waliajiriwa huku asilimia 99 wakiwa Watanzania.

Bwawa lake lina uwezo wa kuhifadhi takribani mita za ujazo bilioni 33 za maji, sawa na karibu mara 10 ya uwezo wa Bwawa la Mtera.

■ Habari

# Jaji Warioba atabiri magumu 2030



Na Mwandishi wetu

MAKAMU wa Kwanza wa Rais (mstaafu) wa Tanzania, Jaji Joseph Warioba ametabiri kuwa Tanzania haitafanya uchaguzi ujao kwa katiba mpya.

Warioba ambaye pia aliwahi kuwa waziri mkuu amesema kwa mtiririko wa matukio unaoendelea sasa kwenye utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Jaji Chande, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa 2029 na Uchaguzi Mkuu wa 2030, utafanyika bila Katiba mpya, hivyo kulazimika kutumia katiba iliyopo kukamilisha chaguzi hizo.

Jaji Warioba alisema utabiri huo unatokana na uzoefu wake, hasa akiangalia msongamano wa matukio na muda uliopo hasa kwa kuzingatia mapendekezo ya Tume ya Jaji Othman Chande, ambayo iwapo yatafuatwa kwa mtiririko kama ilivyoelekezwa.

“Na ikiwa hivyo, tutafika 2029 hatuna Katiba mpya na tutafanya uchaguzi huu wa 2029 na 2030 kwa kutumia Katiba hii hii na tume hii hii ya uchaguzi, na tukifika hapo tutarajie kupata matatizo huenda makubwa kuliko yaliyojitokeza 2025,” amesema.

Jaji Warioba ametoa utabiri huo wakati akizungumza katika kipindi cha Mizengwe, kinachorushwa na Kipindi cha Jenerali Ulimwengu, kuhusu mwelekeo wa utekelezaji wa baadhi ya mapendekezo ya Jaji Chande unaoendelea, hatua inayoonesha serikali imekubali mapendekezo hayo.

Akifafanua, Jaji Warioba alieleza kuwa moja kati ya mapendekezo ni kuwa na tume ya maridhiano, na kwamba ratiba hadi kufikia mwaka 2028 yawe yamekamilika yote pamoja na kuwa na Katiba mpya ili iweze kutumika kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa - 2029 na Uchaguzi Mkuu - 2030.

“Nimefuatilia ratiba ya mapendekezo ya Tume ya Jaji Chande, kwanza ilikuwa kuunda tume ambayo itafanya uchunguzi wa mambo yaliyotokea nani anahusika na tume hiyo imeundwa na imeshaapishwa…”

“Mwanzoni waliteuliwa majaji wa hapa nyumbani lakini sasa wamefikia sita, baada ya kuongeza mmoja kutoka Uganda na mwingine kutoka Namibia ambao wamepewa miezi mitano kufanya uchunguzi na kama ikihitajika wataongezewa muda…”

“Ukimaliza hiyo kuna kamati ya wataalmu kuangalia na kulinganisha Katiba ya sasa, rasimu ya tume ya mabadiliko ya katiba na Katiba iliyopendekezwa na bunge, hatujui watapewa muda gani kuifanya hiyo kazi…”

“Lakini wakimaliza, kutokana na maelezo ya Jaji Chande, watakwenda kwa wananchi kuwauliza na wakifika kwa wananchi siyo suala la muda mfupi, litachukua muda ukishamaliza hilo ndiyo itafanya kuunda tume ya maridhiano,” alisema.

Alisema tume ya maridhiano ikimaliza ratiba yake ndipo utaanza mchakato wa kutafuta katiba mpya, ratiba ambayo yeye binafsi anaiona haiwezekani kuitekeleza katika muda wa miaka miwili na anaamini hata watu ndani ya serikali wakiifuata ratiba hiyo, katiba haitaweza kukamilika mwaka 2028.

Inaendelea Uk. 23

# Jaji Warioba atabiri

Inatoka Uk. 22

"Nikianza na tume ya maridhiano, kuna mambo mengi ambayo lazima kukubaliana na moja, kama Tume ya Jaji Chande ilivyosema, hili ni suala mtambuka ambalo litahusu watu wengi, hii siyo tume ya kawaida ya rais kwamba atateua tume na kuipa hadidu za rejea…"

"Tukiangalia kama tume ya mabadiliko ya Katiba, rais alipata mawazo ambapo watu wengi walisema hawataamini tume ambayo imeteuliwa na rais bila kupata ushauri kwa sababu wanaohusika na matatizo ndio wanataka ushiriki wa watu wengi zaidi ili waweze kutoa mawazo, siyo wachache walioteuliwa," alieleza.

Jaji huyo mstaafu alisema katika hilo wapo wanasiasa, vyama vya siasa, taasisi za kidini, taasisi za kiraia, lakini kuna makundi mengine ambayo yanataka tume ishughulikie masuala hasa ya vijana kwa sababu matatizo tuliyo nayo vijana wakisema wanaandamana unaota serikali inavyochukua hatua.

"Hii siyo rais ateue tu, kwanza apate ushauri, kama anataka wawakilishi kutoka taasisi za kidini awaulize wao wenyewe, kama ni taasisi za kiraia, wenyewe wapendekeze kwa sababu wanajua mawazo yao ni nini, ndiyo ninayosema hiyo…"

"Watakapokutana suala la kwanza ni kutengeneza hadidu rejea zao, wajue ni masuala gani watazungumza na watakayozungumza juu ya Katiba yatakuwapo nayo yatakuwa muhimu. Pia muda wenyewe utakuwa mrefu sasa wasije wakafikiri maridhiano wataweza kuyapata kwa miezi sita…"

"Sasa hivi hatujaweka mazingira ya kuweza kusema ni akina nani watakaoshiriki na ukiona malumbano yanayotokea huna uhakika kwamba wote wanaohusika watashiriki na wakiwepo ambao hawatashiriki tutaendelea na hali kama hiyo…"

"Katika haya maridhiano ni lazima itafutwe njia vijana wawepo na raia wengine, ukichukua kwa mfano masuala yatakayozungumzwa ni pamoja na matatizo yanayowahusu wananchi wenyewe, ambapo ukiangalia kwa sasa hawana uhuru, Watanzania wanaishi kwa woga siyo kama ilivyokuwa," alisema.

> **"Sasa hivi hatujaweka mazingira ya kuweza kusema ni akina nani watakaoshiriki na ukiona malumbano yanayotokea huna uhakika kwamba wote**



Alisema wengi, wanaeleza kuwa wanaogopa kutekwa, kupotea, kwa hiyo hawawezi kutoa maoni kwa kuwa wanaogopa.

Warioba alieleza kuwa inafikirisha zaidi hivi sasa kubainika kuwa watu ambao – angalau wanaweza kuwa huru, wakiwamo wanafunzi wa vyuo vikuu na wahadhiri wanakamatwa na kupewa kesi za uhaini.

"Kuna wakati mimi mwenyewe, kama nilivyowahi kusema niliwahi kupigiwa simu tu kwamba zima simu yako hadi tutakapokwambia, hawakwambii kwa sababu gani wala sheria inayotumika, wakaniita kwenye mkutano nikapigiwa simu usiende," alisema.

### Utendaji wa bunge

Jaji Warioba pia aligusia utendaji wa bunge kwa sasa na kueleza kushangazwa kwake na namna linavyofanya kazi zake, akisisitiza umuhimu wa mgawanyo wa madaraka na kuitenga serikali na bunge.

"Awali tuliwahi kupendekeza wakati ule ila ukiona sasa kwa jinsi serikali ilivyo na nguvu, wabunge wamekuwa ni machawa, kila mmoja akizungumza ni lazima amtaje rais, lakini husikii wakizungumzia watu wao, maana ya ubunge ni kama haipo. Wangekuwa ni wabunge haswa, wangekuwa wanapata mawazo yao kutoka kwa wananchi…"

"Kwa yaliyotokea mwaka jana, watu wengi wa nchi hii wamekufa, lakini hukusikia bunge likizungumzia hili, husikii sauti yake, hivi hawa wabunge huko walikotoka hakuna watu waliouawa?" Alihoji.

Alidai kuwa kwa sasa bunge halina madaraka kamili kwa sababu ya serikali, limemezwa.

Kilinge cha Mawasiliano



Na Loth MAKUZA

# Kuonekana siyo sawa na kuaminika

KUNA jaribio dogo ninalotumia kila ninapokutana na mteja mpya. Namuuliza ataje jambo moja ambalo taasisi yake imewahi kukubali hadharani kuwa ilikosea katika miaka miwili iliyopita.

Wengi hukaa kimya na wengine hucheka kwa woga na wapo wanaosisitiza kuwa hakuna kitu chochote.

Ukimya huo unaniambia zaidi kuhusu hali halisi ya taasisi mbele ya jamii kuliko ripoti yoyote ya takwimu za mitandao inavyoweza kuniambia, kwa sababu taasisi ambayo haijawahi kukosea hadharani kwa kawaida ni ile ambayo haijawahi kuwa ya kweli hadharani pia.

Jaribio hilo dogo linaashiria jambo kubwa zaidi. Taasisi inaweza kuonekana kila mahali, lakini bado ikatiliwa shaka, inaweza kutawala kila jukwaa la mitandao lakini ikapoteza heshima chumbani.

Kuonekana na kuaminika siyo ndugu. Kimoja ni kuhusu kuonekana. Kingine ni kuhusu kuaminiwa.

Kwa zaidi ya muongo mmoja nikifanya kazi katika Uhusiano na Umma na Mawasiliano ya kimkakati, nimeshuhudia taasisi zikimwaga fedha nyingi katika kampeni, mabadiliko ya chapa, na 'kelele za kidijitali,' kisha zikashuhudia uaminifu ukitoweka polepole mlangoni wa nyuma bila wao kutambua.

Mazingira ya kidijitali yanasonga mbele kwa kasi kuliko uwezo wa kuthibitisha ukweli. Watu hawasubiri tena uthibitisho kabla ya kuunda maoni yao, huunda maoni kwanza, kisha hutafuta uthibitisho baadaye.

Kwa hiyo swali la msingi linalowakabili viongozi leo siyo "tufanyeje ili tuonekane zaidi?" bali ni; "tunawezeje kuendelea kuaminika wakati kila mtu mwingine anazidi kupaza sauti?"

Mambo matano yanatofautisha taasisi zinazoweza kufanikisha hili na zile zisizoweza.

Kwanza, mawasiliano lazima yasikike kibinadamu, jamii imejenga uwezo wa kutambua lugha za kishirika zinazolenga kumkinga msemaji badala ya kumjulisha msikilizaji.

Pili, kile taasisi inachosema na kile inachofanya lazima viwiane. Wataalamu wa mawasiliano huita pengo kati ya hivyo viwili "pengo la kusema na kutenda," na katika enzi hii ya kidijitali pengo hilo hujifunga lenyewe hata kama viongozi hawataki.

Utafiti maarufu wa kimataifa wa Edelman Trust Barometer, unaohusisha karibu watu 34,000 katika nchi 28 kila mwaka, unaonyesha kwamba watu wanamwamini mwajiri wao zaidi kuliko wanavyoiamini biashara kwa ujumla au serikali.

Tatu, kasi si hiari tena, zamani ukimya ulinunua muda, sasa unanunua mashaka.

Wachambuzi wanaofuatilia majibu ya migogoro wamegundua kwamba taasisi zinazojibu ndani ya saa moja ya kwanza huhifadhi uaminifu mkubwa zaidi wa umma kuliko zile zinazosubiri hata siku moja tu, na migogoro isiyoshughulikiwa vizuri inaweza kuathiri thamani ya soko karibu papo hapo.

Taasisi zinazopita salama katika wakati mgumu si zile zenye kauli za akili sana, ni zile zilizojitokeza kwanza, kabla mtu mwingine hajaandika hadithi kwa niaba yao.

Nne, mawasiliano yanahitaji nafasi mezani, si kiti karibu na mlango. Kuchukulia Uhusiano na Umma kama pambo badala ya mkakati ni miongoni mwa makosa ya gharama kubwa zaidi ambayo timu ya uongozi inaweza kufanya.

Tano, teknolojia inapaswa kuhudumia uaminifu, si kuubadilisha. Otomatiki na akili bandia ni muhimu kweli katika kufuatilia mazungumzo na kubaini matatizo mapema.

Taasisi ambazo zitaendelea kusimama, na kuaminiwa, miaka mitano ijayo hazitakuwa lazima zile zenye sauti kubwa zaidi chumbani.

Zitakuwa zile zilizogundua mapema kwamba kuonekana ni rahisi, lakini kuaminiwa lazima kupatikane upya kila siku.

***Mwandishi wa safu hii ni mtaalamu wa Uhusiano na Umma (PR). Anapatikana kwa namba: 0625 704 995 na kupitia email; projects@lothmakuza.co.tz***

Na Emmanuel JACOB



# Kwa nini viungo bandia vya msaada hutupwa?

MARA nyingi tunasikia na hata kuona wafadhili kutoka nchi zilizoendelea wakigawa viungo bandia vya bure kwa watu wenye ulemavu katika nchi zinazoendelea.

Kitendo hiki huonekana kama cha huruma na upendo, lakini swali la msingi tunalopaswa kujiuliza ni hili; Kwa nini sehemu kubwa ya misaada hii huishia kutupwa, kutelekezwa na kugeuka kuwa takataka?

Uchunguzi unaonyesha kuwa kutotumika kwa viungo hivi bandia hakusababishwi tu na dharau ya wapokeaji, bali ni matokeo ya mifumo isiyokidhi mahitaji halisi na mazingira ya wapokeaji.

Kwa wasomaji wa safu hii ni muhimu sana tufahamu haya; kwamba sehemu inayounganisha kiungo bandia na mwili wa binadamu inahitaji kutengenezwa kulingana na umbo halisi la mhusika.

Viungo vya msaada vilivyotumiwa tayari (mtumba) au vilivyotengenezwa kwa vipimo totauti hali inayosababisha maumivu makali, michubuko na hata majeraha kwenye ngozi.

Vilevile sehemu ya mwili iliyobaki hubadilika umbo na kupungua ukubwa kadiri muda unavyokwenda.

Kiungo cha bure kisichoweza kurekebishwa kinakuwa cha purukushani na hatimaye kuachwa.

Hata hivyo, vifaa vingi vya msaada ni vizito na havijatengenezwa kwa ajili ya hali ya hewa ya joto. Hali hii husababisha jasho jingi na kero kubwa kwa mtumiaji.

Kumpa mtu kiungo bandia kisichomtosha ni sawa na kumlazimisha kutembea siku nzima akiwa amevaa kiatu kilicho kidogo kwa namba mbili. Mwishowe, ataamua kutembea peku.

Misaada mingi hutoka nchi za Ulaya ikiwa na teknolojia ya hali ya juu au iliyoundwa kwa ajili ya mazingira ya mjini yenye miundombinu iliyoendelea.

Vifaa hivi maridadi hushindwa kuvumilia mazingira ya vijijini kwenye miinuko, tope na njia zisizo rasmi. Matokeo yake, vinavunjika haraka sana.

Mara nyingi, nchi maskini hugeuzwa sehemu ya kutupia vifaa vilivyochakaa au vilivyopitwa na wakati ambavyo havina hata viwango vya usalama.

Tatizo kubwa zaidi la misaada hii ni mtazamo wa “saidia na uondoke” (give and go). Vifaa vinatolewa bila kuwepo kwa mfumo wa usaidizi wa muda mrefu. Pindi kifaa kinapoharibika, mtumiaji kupata kipuri cha kubadilisha inakuwa ni vigumu. Na maeneo mengi ya vijijini hayana wataalamu waliosomea, ambao hukarabati, au kuwafundisha watumiaji jinsi ya kutumia viungo hivyo kwa usalama.

Dhana kwamba “cha bure hakithaminiwi” inapotosha ukweli katika suala la viungo bandia.

Watu hawavitelekezi vifaa hivi kwa sababu vilikuwa bure, bali kwa sababu vinasababisha maumivu, havina msaada wa kiufundi, na havilingani na maisha yao ya kila siku.

Msaada wa kweli sio kuleta makontena ya vifaa vilivyotumika visivyokidhi viwango. Msaada wa kweli ni kuwekeza kwenye miundombinu ya ndani: kufundisha wataalamu wa ndani, kutengeneza viungo bandia kwa kutumia malighafi za eneo husika, na kuhakikisha huduma za marekebisho zinapatikana karibu na jamii.

***Mwandishi: Emmanuel Jacob, Afisa Mfiziotherapia (Mwenyekiti wa Tanzania Physiotherapy Initiative). Simu: 0765359305 Instagram: Emmanuel Jacob.***



Bustani ya Sheria



Na Wakili Karim Gabriel Mussa

# Sakata la Wakili Fatma Karume – IV

KATIKA sehemu ya tatu tuliona jinsi Kamati ya Maadili ya Mawakili ilivyomkuta Wakili Fatma Karume na hatia ya utovu mkubwa wa nidhamu na kuamuru afutwe kabisa kwenye Daftari la Mawakili.

Kwa wengi, huo ulionekana kuwa mwisho wa safari yake ya uwakili, lakini kwa Fatma Karume Ilikuwa mwanzo wa vita vipya vya kisheria.

Fatma alikata rufaa Mahakama Kuu baada ya kuvuliwa uwakili kwani hakukubaliana na uamuzi wa kamati.

Kupitia wakili wake, Peter Kibatala, mbele ya Jopo la Majaji watatu (Full Bench), hata hivyo kabla hata rufaa haijaanza kusikilizwa, serikali iliweka mapingamizi ya awali.

Upande wa Mwanasheria Mkuu uliiambia Mahakama kwamba rufaa ya Fatma ilikuwa mbovu kisheria. Walidai kwamba hakufuata utaratibu wa kutoa Notice of Appeal na kwamba alitumia hati isiyo sahihi kwa kuwasilisha Petition badala ya Memorandum, au kinyume na utaratibu uliowekwa kwenye Kanuni za Nidhamu za Mawakili na zaidi kuwa hakufuata njia sahihi ya kuwasilisha rufaa kupitia Katibu wa Kamati kama sheria ilivyotaka.

Kwa kifupi, serikali ilitaka Mahakama isisikilize kabisa hoja za Fatma nah apo jopo la majaji likachambua hoja hizo moja baada ya nyingine.

Baada ya kufanya hivyo likasema kuwa mapingamizi yote hayana msingi wa kuizuia rufaa kusikilizwa. Mahakama ikaamua kwamba kasoro zilizodaiwa hazikuwa za kiwango cha kuua rufaa.

Kwa hiyo, rufaa ya Fatma ikaendelea kusikilizwa kwa hoja zake za msingi na hii ikawa ushindi wake wa kwanza tangu avuliwe uwakili, ingawa ushindi mkubwa ulikuwa bado mbele.

Hoja iliyoitikisa kesi nzima ya Fatma ni kuwa hakujikita kujitetea kuhusu kama maneno aliyotumia yalikuwa sahihi au la, badala yake aliuliza swali moja muhimu sana. Je, Kamati ya Maadili ilikuwa na mamlaka ya kusikiliza shauri lililofikishwa mbele yake kwa namna lilivyofikishwa?

Hii ndiyo hoja iliyogeuza kabisa mwelekeo wa kesi. Kupitia Wakili Peter Kibatala, Fatma aliieleza Mahakama ya Tanzania kuwa katika kesi ya Ado Shaibu, Jaji Feleshi alikuwa tayari ametoa maelekezo maalumu. Maelekezo hayo yalikuwa wazi kabisa. Kwamba Msajili wa Mahakama Kuu ndiye alitakiwa kupeleka suala la nidhamu la Fatma kwenye Kamati ya Maadili.

Lakini kilichotokea baadaye kilikuwa tofauti. Badala ya kusubiri Msajili atekeleze amri ya Mahakama, Mwanasheria Mkuu wa Serikali akaenda mwenyewe kufungua shauri jipya mbele ya Kamati ya Maadili. Kwa hiyo Fatma akasema, Kamati ilisimamia shauri ambalo halikuletwa mbele yake kwa utaratibu ulioagizwa na Mahakama.

Na kama msingi wa kuifikisha kesi ulikuwa batili, basi hata uamuzi wote uliotolewa ulikuwa batili.

Serikali haikukubalia  na ilisema kuwa Mahakama ilikuwa imetoa maelekezo kwa Msajili, lakini maelekezo hayo hayakumzuia Mwanasheria Mkuu kufungua malalamiko mengine mapya.

Zaidi ya hayo malalamiko yaliyowasilishwa mbele ya Kamati hayakuhusu maneno yaliyotamkwa Mahakamani pekee, yalijumuisha pia machapisho ya Twitter na matukio mengine yaliyotokea baadaye.

Kwa hiyo, kwa mtazamo wa serikali, Kamati ilikuwa na mamlaka kamili ya kuyasikiliza.

### Uamuzi wa Mahakama

Baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili, jopo la majaji likafikia hitimisho ambalo halikutarajiwa na wengi.  Majaji wakasema; ni kweli Mahakama ya kwanza ilikuwa tayari imetoa agizo mahsusi kwamba Msajili wa Mahakama ndiye angepeleka suala hilo kwenye Kamati.

Agizo hilo lilikuwa bado halijawahi kufutwa wala kubadilishwa.

Kwa hiyo, Mwanasheria Mkuu hakuwa na mamlaka ya kulipuuza agizo hilo na kufungua shauri jipya lililochanganya malalamiko yaleyale yaliyokuwa tayari yameguswa na Mahakama.

Majaji wakasema hatua hiyo ilikuwa imeenda kinyume na agizo la Mahakama. Na pale ambapo msingi wa kuanzisha shauri ni batili, na kwamba hata uamuzi unaotolewa juu yake hauwezi kusimama.

Itaendelea…

***Mwandishi ni Mwanasheria na Mchambuzi wa Sheria kutoka KGM Attorneys). Anapatikana kwa namba: 0755 395 572 au Email: karimbinmussa@gmail.com***



Na Rashid MTAGALUKA

Hoja Yangu

# Kizimkazi: Kutoka siku ya mtaa hadi jukwaa la taifa

KUNA matukio huanza kama wazo dogo la jamii, lakini baadaye hukua na kuwa sehemu ya utambulisho mpana wa taifa. Tamasha la Kizimkazi ni miongoni mwa mifano hiyo.

Kilichoanza mwaka 2015/2016 kama tukio la kuwaaga wananchi wa Kizimkazi baada ya Dk. Samia Suluhu Hassan kuteuliwa kuwa mgombea mwenza wa urais, baadaye kikajulikana kama Samia Day, kisha Kizimkazi Day, leo ni tamasha linalovuka mipaka ya eneo hilo.

Mwaka 2020 liliingia rasmi katika sura ya tamasha, likipanua maudhui yake kutoka utamaduni kwenda utalii, uwekezaji na maendeleo ya jamii.

Hapo ndipo nguvu kubwa ya Kizimkazi ilipo. Si tena suala la wakazi wa Kizimkazi kujikusanya kwa ajili ya kusherehekea utamaduni wao, bali ni jukwaa linalowakutanisha wananchi kutoka Zanzibar na Tanzania Bara, wafanyabiashara, wawekezaji, taasisi za Serikali, wasanii na wageni kutoka nje ya nchi.

Rais Samia mwenyewe mwaka 2024 alieleza kuwa tamasha hilo limekua kutoka tukio la jamii hadi kuwa la kitaifa na kuelekea kimataifa.

Tamasha la mwaka huu limeendelea kuthibitisha mwelekeo huo. Limeambatana na uzinduzi wa miradi tisa ya maendeleo, ikiwamo kituo cha mafunzo ya ufundi, mradi wa maji, uwanja wa watoto na maboresho ya miundombinu ya jamii. Hii inaonesha kuwa tamasha linaweza kuwa zaidi ya burudani; linaweza kuwa chombo cha kuunganisha sherehe na maendeleo.

Lakini mafanikio yake makubwa zaidi yanapaswa kupimwa kwa kile kinachobaki baada ya muziki kuzimwa na wageni kuondoka. Je, wafanyabiashara wadogo wanapata soko? Je, vijana wanapata ajira na ujuzi? Je, utalii wa Kusini Unguja unaongezeka? Je, wawekezaji wanaona fursa mpya?

Haya ndiyo maswali muhimu kwa sasa.

Kizimkazi tayari imeonyesha kuwa utamaduni unaweza kuwa mtaji wa uchumi. Maonesho, michezo, muziki, vyakula vya asili, utalii na shughuli za baharini vinaweza kuunganisha historia ya eneo na fursa za kisasa.

Ushiriki wa wageni na wasanii kutoka nchi jirani, ikiwamo Uganda, unaonesha pia uwezo wa Kizimkazi kuwa daraja la mwingiliano wa kitamaduni Afrika Mashariki.

Kwa hiyo, Kizimkazi haipaswi kubaki kuwa tamasha la siku chache. Inapaswa kujengwa kuwa brand ya utalii na utamaduni ya Tanzania, yenye kalenda ya mwaka mzima, kuvutia wawekezaji na kuhakikisha wananchi wa eneo husika ndio wanakuwa wanufaika wakuu.

Kutoka Samia Day hadi Kizimkazi Festival, safari hii imetufundisha jambo moja; wazo dogo la jamii linaweza kuwa jukwaa kubwa la taifa, ikiwa linaendelezwa kwa maono na tija.

***Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com***



*Rais Samia akiwa na mwanamuziki wa Uganda, Jose Chameleon kwenye Tamasha la Kizimkazi.*

■ Habari

# HERO yawekeza ulinzi, usalama wa mtoto



*Mtendaji Mkuu wa HERO, Joseph Kayinga*

Na Mwandishi WETU

MALEZI bora katika makuzi ya mtoto ni msingi wenye afya, mafanikio na ustawi kwa jamii inayojitambua.

Hakika ni kwamba mtoto anayelelewa kwa upendo, nidhamu na maadili hukua akiwa na tabia njema, hekima na mwenye kujitegemea kifikra mapema.

Kupitia malezi hayo, jamii hupanda mbegu za uaminifu, bidii na huruma ambazo baadaye humfanya mtoto awe raia na ama kiongozi mwema.

Mtoto anayelelewa vizuri leo ndiye atakayejenga taifa bora la kesho.

Kwa kutambua hilo, Taasisi ya Health and Education at Risk Organization (HERO), imeanza kuhamasisha jamii na hasa wazazi, kuwajibika katika malezi sahihi ya watoto, ikiwa na lengo la kupunguza wimbi la watoto wanaojilea wenyewe na wanaofanya kazi mitaani.

Mtendaji Mkuu wa HERO, Joseph Kayinga, anasema lengo jingine la kampeni hiyo ni kupambana na umaskini wa kipato, fikra hasi na maisha bwete.

"Shauku yetu ni kuongeza tija ya watu wetu kwa kutumia taaluma ya ustawi wa jamii uzalishaji mali na kipato, kupitia kilimo, biashara na ufugaji," anasema.

Katika kipindi cha wiki mbili zilizopita, asasi hiyo imekuwa ikishughulikia mashauri matatu katika kata za Mabibo, Mbweni Mabwepande na Bunju jijini Dar es Salaam.

Mashauri hayo yanalenga kuimarisha usalama wa mtoto na kuhakikisha anapata ulinzi unaostahiri na malezi bora kutoka kwa wazazi wote wawili.

"Katika kuhakikisha kila mtoto anapata malezi yanayofaa, hata watoto wanaokutwa na changamoto ya kubaki kwenye familia, serikali inaagiza kwamba mtoto huyo atasaidiwa kwa kupelekwa kwenye makao ya kulea watoto wenye changamoto baada ya juhudi nyingine zote za kuhudumiwa akiwa kwenye familia ya asili kushindikana," amesema Kayinga.

Sambamba na hilo, anasema asasi yake imepanua ushirikiano wa kimataifa kwa kutekeleza miradi miwili ya kimkakati ya kimataifa itakayohusisha nchi tano; mbili zikiwa Afrika na zinazosalia nje ya Afrika.

"Mradi mkuu unajulikana kama, International Social Workers Exchange Partnership - ISWEP ambao ulianza mwaka 2018 kwa kushirikiana na wataalamu wa Ustawi wa Jamii wa Jiji la Hamburg, Ujerumani.

Anaongeza kuwa mpango huo umekuwa ukilenga ubadilishanaji wa maarifa baina ya wataalamu wa ustawi wa jamii.

Anaeleza kuwa tangu kuanza kwa mpango huo mwaka 2018, wataalamu wa ustawi walioshiriki walinufaika kwa viwango tofauti, lakini pia taasisi na vituo vilivyohusishwa vilipata uzoefu kila kimoja kwa namna yake.

Anataja changamoto kadhaa zilizojitokeza na pia kulikuwa ukiukwaji wa maadili nje ya utaratibu uliowekwa kiasi cha kusababisha asasi yake kukemea wahusika na hata kuchukua hatua za haraka pamoja na uchunguzi wa kina.

Kati ya hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kubadilisha utaratibu kwa kutunga sera na miongozo mipya ya usimamizi na uteuzi wa washiriki.

# Jaji Mshibe asisitiza maandalizi kukabili athari za elnino




*Mwenyekiti wa Bodi ya TMA, Jaji Mshibe Ali Bakari*

**Na Mwandishi wetu**

MWENYEKITI wa Bodi ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Jaji Mshibe Ali Bakari, amezitaka sekta zote nchini kutumia ipasavyo taarifa za mamlaka hiyo kufanya maandalizi ya kisekta ya kukabili athari zinazoweza kusababishwa na uwepo wa elniño.

Jaji Mshibe aliyasema hayo wakati akifungua Mkutano wa 25 wa kujadili Utabiri wa Msimu wa Mvua za Vuli, Oktoba hadi Desemba 2026, uliofanyika mwishoni mwa wiki katika Ukumbi wa Mikutano wa PSSSF, Dodoma.

"Tunapojiandaa kupokea taarifa ya utabiri wa mvua za vuli, Oktoba hadi Desemba 2026, ni muhimu kila mmoja wetu kufuatilia kwa karibu na kuelewa taarifa hizo ili kuanza maandalizi ya hatua za kuchukua kukabiliana na athari za hali ya hewa zinazotarajiwa kujitokeza katika sekta yake, kwa kutambua kuwa upo uwezekano mkubwa kwa elniño kuendelea kuimarika kuelekea mwishoni mwa mwaka 2026," alisema Jaji Mshibe.

Alisema Tanzania, kama ilivyo kwa nchi nyingine duniani, inaendelea kukabili athari za mabadiliko ya hali ya hewa yanayodhihirishwa kupitia ongezeko la joto, ukame, upepo mkali, vimbunga na vipindi vya mvua kubwa vinavyoweza kusababisha mafuriko.

Mkurugenzi Mkuu wa TMA na Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi, Dkt. Ladislaus Chang'a, alisema TMA imeendelea kuboresha utoaji wa taarifa za hali ya hewa, ikiwemo kuandaa utabiri mahsusi kwa maeneo madogo kwa wilaya 86 zilizopo katika mikoa inayopata mvua za vuli.

Aidha, Dkt. Chang'a alisisitiza kuwa taarifa za utabiri na tahadhari zinapaswa kuzingatiwa katika sekta zote za kiuchumi na kijamii, kwa lengo la kuongeza tija na kupunguza madhara yanayoweza kusababishwa na hali mbaya ya hewa itakayotokana na uwepo wa el nino nchini.

"Nitumie fursa hii kuwajulisha kuwa mwaka huu 2026 tunakabiliwa na changamoto ya elnino ambayo inatarajiwa kuendelea kuimarika kuelekea mwishoni mwa mwaka na hivyo kuchagiza mvua za vuli, hivyo basi matumizi sahihi na kwa wakati ya taarifa za hali ya hewa ni muhimu kwa Kila sekta katika kukabiliana na changamoto hii," alisema Dkt.Chang'a.

Naye, mwakilishi wa wadau mbalimbali kutoka Zanzibar, Makame Makame, akiwa Mkurugenzi wa Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar, alisema utabiri wa hali ya hewa ni jambo muhimu zaidi hasa katika kipindi cha el nino ambapo jamii na sekta zote muhimu zinahitaji kujikinga, kujiandaa, kukabiliana na majanga au maafa yanayoweza kutokea sambamba na kurejesha hali baada ya maafa.

Mkutano huo uliobeba kaulimbiu; "Kupunguza Pengo la Uelewa wa Tahadhari za Hali ya Hewa kwa Pamoja." Ulihusisha pia utoaji wa mrejesho kutoka kwa wadau kuhusu utabiri wa msimu wa mvua za Masika uliokuwa na usahihi wa asilimia 94.1".

# Barua za Wasomaji



**Tunakaribisha barua. Tuma kupitia**

**Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba; +255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@pambazuko.or.tz**

## Mamlaka ishughulikie kero ya ombaomba Dar

**Mhariri,**
JIJI la Dar es Salaam limejaa watu wanaoomba msaada mitaani, hasa kwenye taa za barabarani na vituo vya mabasi.
Wengi wao ni watoto na wazee waliolazwa na umaskini, hali inayoleta usumbufu kwa madereva na abiria kwani wengine huingia barabarani na kuzuia magari.

Ombaomba hao pia hasa watoto wamekuwa wakijihusisha na vitendo vya uhalifu wanavyovifanya kwa kivuli cha uombaji.

Tunaomba mamlaka kwa kushirikiana na wadau vishughulikie jambo hili ili kuondoa kero hizo.

Lakini pia Jeshi la Polisi lifanye doria ili kudhibiti uwepo wao na wananchi waache kutoa msaada mtaani bali tuwafikishie vituoni. Hii itasaidia kupunguza kero na kulinda heshima ya jiji letu.

**Habiba Hamidu,**
**Dar es Salaam.**

## Wapiga debe wadhibitiwe

**Mhariri,**
NAANDIKA barua hii kwa kulaani uwepo wa wapigadebe katika vituo vya daladala kwa sababu wamekuwa kero kubwa kwa abiria.

Wengi wao hupiga kelele na kutoa matusi ili kuvuta abiria, hasa kwenye vituo na masoko.

Wengine hupanda mabasi hata wakati basi likiwa limejaa na kusababisha msongamano na ajali ndogo ndogo. Tabia hii imepunguza heshima ya usafiri wa umma na kuwafanya watalii kuhisi kutokuwa salama.

Tunaomba Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (Latra) kwa kushirikiana na halmashauri na mamlaka za serikali za mitaa kuweka mifumo ya kupokea abiria iliyo na nidhamu.

Pia Jeshi la Polisi lifanye doria ili kuwadhibiti wapiga debe hawa.

Ikiwa watadhibitiwa watasaidia jiji kuwa tulivu na lenye utaratibu na heshima hasa katika maeneo ya vituoni.

**Jackson Peter, Makongo- Dar es Salaam**

## Serikali iokoe Stendi ya Mtoni Kijichi

**Mhariri,**
NATOA wito kwa serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na Mamlaka ya Dar es Salaam kuja kuangalia kilio chetu sisi wakazi wa Mtoni Kijichi.

Miaka michache iliyopita serikali ilitumia fedha nyingi kujenga stendi ya mabasi ya kwenda mikoa ya kusini iliyopo Mtoni Kijichi.

Lengo lilikuwa kupunguza msongamano jijini, kuwapunguzia abiria usumbufu na kutoa huduma bora.

Leo stendi hiyo imetelekezwa na kubaki bila kazi yoyote na kusababisha uwekezaji wa mamilioni kupotea bila tija yoyote.

Abiria wanaokwenda mikoa ya kusini hivi sasa wamerejea tena katika eneo la Mbagala na Temeke, ndio wanateseka kusubiri mabasi ya kwenda kusini wakipigwa na jua au kunyeshewa mvua kwa sababu stendi hizo hazina miundombinu yoyote.

Swali langu ni kwa nini kujenga mradi mkubwa kisha kuutelekeza? Hii ni kupoteza fedha za walipakodi.

Naiomba serikali ifanye ukaguzi, irekebishe stendi hiyo na ianze kuitumia mara moja na ikiwa inaona haifai kwa kazi hiyo wawekeze. Pia iwajibishe waliotelekeza mradi huu.

Watanzania tunataka kuona matunda ya miradi mbalimbali kwa manufaa ya wananchi.

**Abiria Mkereketwa,**
**Dar es Salaam.**


MOVE FOR DISABILITY
INCLUSION BY DESIGN 26'
WALK
with Us
29th August 2026
SPONSERED BY circleg
Kua mshiriki kwa Tshs 40,000/- Tu!
Nunua ticket yako kutumia Lipa Namba
MOVE FOR DISABILITY
6 1 2 4 6 6 1 0
INCLUSION BY DESIGN 26'
SPONSERED BY
UHURU
circleg
Pambazuko

Makala

# Stadi za maisha zinavyochochea ustawi wa Watanzania



Watende Ramadhani

Na Greyson MGOI

WATENDE Ramadhani Botea, miaka 44, malezi bora hayatoshi kwa chakula, mavazi na elimu. Mtoto anahitaji pia uwezo wa kufikiri, kujiamini, kuwasiliana na kutatua changamoto za kila siku.

Watende, mkazi wa Makulunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Shule ya Msingi Migiro wilayani Bagamoyo, Pwani, anasema mafunzo yanayotolewa na Uwezo Tanzania yamebadili mtazamo na mbinu zake za malezi.

Kabla ya hapo, hakuelewa maana ya stadi za maisha wala nafasi yake katika ukuaji wa mtoto. Kupitia Mradi wa Stadi za Maisha na Maadili Afrika Mashariki (ALiVE), alitambua kuwa ni mahiri wezeshi za kukabiliana na mazingira na changamoto za kila siku.

Mafunzo yalimjengea uelewa kuhusu mawasiliano, ushirikiano, kujiamini na utatuzi wa matatizo. Anaamini mtoto hapaswi kupewa kila jibu, bali aongozwe kulifikiria tatizo, kuchunguza chanzo na kupendekeza suluhisho.

"Nilijifunza kuwa unapokabiliwa na tatizo, hatua ya kwanza ni kulitambua vizuri. Baada ya hapo unafikiria njia mbalimbali za kulitatua na kuchagua inayofaa zaidi," anasema.

Maarifa hayo ameyahamishia kwa watoto wake. Badala ya kuingilia kati haraka, huwauliza wanaweza kuikabili vipi changamoto. Njia hiyo imewajengea ujasiri, kujiamini na kufanya maamuzi.

Watende aliwashirikisha wazazi wengine kupitia mikutano ya kijiji na wengi wakavutiwa. Anasema wazazi wana wajibu wa kukuza stadi hizi kwa watoto kwa sababu ndizo huweka msingi wa malezi bora.

Katika kukuza utatuzi wa matatizo, wazazi walifundishwa kuwaacha watoto wajaribu kukabili changamoto kulingana na umri wao. Mtoto akileta tatizo, mzazi amuulize: "Unafikiri unaweza kulitatua vipi?" Kisha amsaidie kutafuta taarifa, kupendekeza njia, kuchagua mbinu na kuijaribu. Ikishindwa, atafakari sababu na njia mbadala.

Watende anaiomba Serikali na jamii kuhakikisha elimu hiyo inawafikia wazazi na watoto wengi zaidi. Bagamoyo pekee, zaidi ya wazazi vinara 40 walipata mafunzo na baadaye kuwafikia wenzao.

"Elimu ya stadi za maisha na maadili ni muhimu kwa kila mtu. Watoto wote wanapaswa kufundishwa shuleni na nyumbani," anasisitiza.

Ripoti ya utekelezaji ya mwaka 2025 inaeleza kuwa kampeni ya wiki 10 iliendeshwa na Uwezo Tanzania, OCODE, Milele Zanzibar na SAZANI Trust. Ililenga kuimarisha ushiriki wa jamii katika kuwajengea watoto uwezo wa kutatua matatizo na kukuza udadisi, ubunifu, ustahimilivu na ujifunzaji endelevu.

Kampeni iliwahimiza wazazi kuruhusu watoto kuuliza maswali na kufikiri kwa kina. Shughuli za vitendo, sanaa na michezo zilitumika kujenga kujiamini na uwezo wa kubuni suluhisho mbadala.

Zanzibar, watu 3,144 walifikiwa moja kwa moja; wanaume 1,063 na wanawake 2,081. Walikuwamo wazazi 949, wanafunzi 1,917, walimu 193, viongozi wa dini 30 na wadau wengine. Wazazi 2,607 walifikiwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja.

Inaendelea Uk. 33

# Stadi za maisha...

Inatoka Uk. 32

Bagamoyo, wazazi 1,464 walielimishwa, pamoja na wanafunzi 40 wa Shule ya Msingi Nianjema, wanafunzi 54 wa Chuo cha Baqwina, wanachama 92 wa vikundi vya akiba na waumini 239. Wanajamii zaidi ya 15,000 walifikiwa kupitia vyombo vya habari.

Matokeo yalionekana katika familia na shule. Baadhi ya wazazi walianza kuwashirikisha watoto katika majadiliano kuhusu maamuzi ya kifamilia na kuboresha mawasiliano nyumbani. Wengine waliacha adhabu kali na kutumia mwongozo chanya, unaowapa watoto nafasi ya kuuliza maswali na kueleza mawazo yao.

Pia, wazazi waliongeza mahudhurio katika mikutano ya shule, kufuatilia maendeleo ya kitaaluma na kuwasaidia watoto kujifunza nyumbani. Kwa wanafunzi, ripoti ilibaini kuimarika kwa udadisi, fikra makini, tabia ya kusoma na kuchambua vitabu, uwezo wa kujieleza, ubunifu na utatuzi wa matatizo. Mahudhurio shuleni yaliongezeka baada ya utoro na kuchelewa kupungua.

Mtaalamu wa saikolojia kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dkt Daniel Marandu, anasema mtoto anapozaliwa na kukua huhitaji maarifa ya kumsaidia kukabiliana na changamoto. Maarifa hayo ndiyo stadi za maisha. Kwa maelezo yake, watoto wenye kiwango kikubwa cha stadi hizo wana nafasi nzuri zaidi ya kufanikiwa kuliko wenye kiwango kidogo.

Naye Ofisa na Mtaalamu wa Mitaala kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Mwanahamisi Jokolo, alieleza mwaka 2025 kuwa ushirikiano kati ya TET na mashirika yasiyo ya kiserikali unaweza kusaidia kukuza stadi za maisha na maadili kwa wanafunzi.

Kupitia mradi wa ALiVE, Uwezo Tanzania na washirika wake wamefanya kazi na wizara zinazohusika na elimu Tanzania Bara na Zanzibar, TET na taasisi nyingine. Ushirikiano huo umechangia kuingizwa kwa stadi za maisha katika mtaala ulioboreshwa na kuwajengea walimu uwezo wa kuzifundisha.

Umuhimu wa hatua hiyo unaungwa mkono na utafiti wa mwaka 2015 wa Jumuiya ya Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki. Ulibaini kuwa wahitimu wengi walikuwa na maarifa ya kitaaluma, lakini walikosa uwezo wa kuyatumia kazini. Waajiri walitaja mapungufu katika mawasiliano, ubunifu, kujitambua, utatuzi wa matatizo na fikra tunduizi. Tanzania, wahitimu sita kati ya 10, sawa na asilimia 61, walionekana kukosa stadi hizo muhimu, hali iliyopunguza nafasi zao za kuajiriwa.


Wanawake wakifundishwa stadi za maisha.

Utafiti wa ALiVE wa mwaka 2022 pia ulionyesha kuwa shule zina mchango mkubwa katika ukuaji wa stadi za maisha. Vijana wa madarasa ya juu, hasa sekondari, walionyesha umahiri mkubwa zaidi kuliko waliokuwa katika ngazi za chini za elimu.

Ushahidi huo umechangia maboresho ya elimu nchini. Mtaala ulioboreshwa, ulioanza kutumika Januari 2024, umezipa stadi za maisha nafasi katika masomo mbalimbali. Miongoni mwazo ni fikra tunduizi, utatuzi wa matatizo, mawasiliano na ushirikiano.

Lengo ni kumjenga mwanafunzi anayeweza kutumia elimu yake kukabili hali halisi za maisha, kujenga mahusiano bora, kubuni ajira, kushirikiana na jamii tofauti, kukuza uchumi na kuimarisha amani.

Simulizi la Watende linaonyesha kwamba mageuzi hayo hayawezi kubaki darasani pekee. Mzazi, mlezi, mwalimu na jamii lazima washirikiane kumjenga mtoto anayeweza kuuliza, kufikiri, kujaribu na kujifunza kutokana na makosa.

Hapo ndipo elimu inapogeuka kuwa nyenzo ya kujenga kizazi chenye maarifa, ujasiri, uwajibikaji na suluhisho endelevu.

Swali linabaki: wewe kama mzazi au mlezi unafanya nini kumsaidia mtoto wako kukuza stadi hizi muhimu za maisha? Na umejifunza nini kutokana na makala haya? Tuma maoni yako kupitia anuani ya mhariri wa gazeti hili.

# ‘Maajabu’ ya Rais Mobutu akiwa Ikulu



Na Mwandishi WETU

MOBUTU SeseSeko Kuku Ngwendu Wazambanga aliwahi kuwa Rais wa Zaire, ambayo sasa inaitwa Jamhuri ya Kidemokrasia na Congo – DRC.

Jina halisi alilopewa na wazazi wake ni Joseph Désiré Mobutu. Baadaye, kutokana na mbwembwe zake, alijiongezea majina mengine.

Alizaliwa Oktoba 14, 1930 katika Mji wa Lisala, wakati huo nchi hiyo ikiwa ni koloni la Ubelgiji, ikijulikana kwa jina la Zaire. Lugha yake kuu ni Lingala, ingawa katika baadhi ya maeneo, hasa mijini, Kifaransa kinazungumzwa zaidi.

Wakongo wengi wanamkumbuka Rais Mobutu kuwa ni kiongozi mwenye kiburi, tamaa, mpenda sifa, mlafi na mroho wa madaraka.

Alipochukua madaraka ya nchi alifanya chochote alichopenda na kuwataka raia wake wafanye alichopenda na kumfurahisha yeye.

Eneo hilo alilozaliwa lipo ndani ya Jimbo la Mongala na Mji wa Lisala ndio mji mkuu wa jimbo hilo na ulipewa hadhi ya kuwa mji mkuu kuenzi historia ya Mobutu ambaye alijenga kasiri la kifahari eneo ambalo kilizikwa kitovu chake na lilipo kaburi la baba yake mzazi.

Mobutu alipenda kwenda kwenye eneo hilo kupumzika na baadaye kujenga kasiri kubwa kule Gbadolite, eneo alikokulia na kulelewa na mama yake; eneo lile kwa sasa lipo ndani ya Jimbo la Nord Ubangi. Mama yake; “Mama Yemo” alizikwa huko na Mobutu aliamua kujenga uwanja mkubwa wa ndege na kuanzisha mbuga ya wanyama ambako sherehe zake zote za kifahari alizifanyia hapo.

Pia katika eneo la Lisala, ndipo Mobutu alipenda kufanya kazi zake na mara nyingi alitumia eneo hilo kutangaza uamuzi mgumu kuhusu nchi.

Moja ya uamuzi mgumu unaokumbukwa kufanywa pale ni kutoa hukumu ya kifo kwa Pierre Mulele kwa kukatwa katwa vipande.

### Maisha na ndoa

Katika uhai wake Mobutu alipata watoto 21 ambao alieleza anawatambua, aliwahi kuoa mara mbili katika ndoa rasmi. Ndoa yake ya kwanza ni binti wa ujana wake, Marie-Antoinette, ambaye alifariki dunia kwa tatizo la moyo Oktoba 22, 1977 huko Genolier, Switzerland, akiwa na umri wa miaka 36 tu.

Baada ya hapo Mobutu alioa Mei 1, 1980, ambapo alifunga ndoa na Bobi Ladawa, mwanamke mrembo kutoka Bandundu.

Siku ya harusi yake, Papa John Paul II alikuwa na ziara ya kuitembelea Zaire (sasa DRC), Mobutu alimkaribisha Papa awe mgeni rasmi katika sherehe za harusi yake ingawa Papa alikataa.

Inaendelea Uk. 35

# 'Maajabu' ya Rais...

**Inatoka Uk. 34**

Jambo lisilojulikana kwa watu ni kwamba siku hiyo Mobutu alioa wanawake wawili kwa siku moja, yaani mtu na pacha wake, Bobi Ladawa na Kosia Ladawa; na ndoa hiyo ilitambulika kama ndoa moja.

Watoto wengi wa Mobutu wapo Kinshasa mpaka sasa na wengine wanaishi Ulaya, kati ya watoto wake wawili wa kiume aliowapata katika ndoa yake ya kwanza walifariki Mobutu akiwa madarakani ambao ni Nyiwa aliyefariki Septemba 16, 1994 - anatajwa kufariki dunia kwa maradhi yanayotokana na Ukimwi, na Konga alifariki mwaka 1992.

Wengine wawili walifariki kwa kufuatana katika kipindi ambacho Mobutu akiwa amefariki dunia. Hao ni Kongulu aliyefariki Septemba 24, 1998 na Manda aliyefariki Novemba 27, 2004.

Watoto wake wengine ni Nzanga Mobutu Ngbangawe, ambaye ni mtoto mkubwa kwenye ndoa yake ya pili, kwa sasa ndiye amebaki kuwa msimamizi mkuu wa familia ya Mobutu.

Nzanga Mobutu aliwahi kugombea urais kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2006, hata hivyo hakushinda na baadaye alifanya kazi kwenye Serikali ya Joseph Kabila, akiwa waziri wa nchi anayeshugulikia kilimo.

Mtoto mwingine ni binti aitwaye Yakpwa (wakongo hupenda kumwita Yaki), huyu ameolewa huko Ubelgiji na mtu anayeitwa Pierre Janssen.

Yakpwa ni mwandishi wa vitabu na ameandika kitabu cha maisha ya Mobutu kinachoitwa "Mobutu's lifestyle in vivid detail" ikimaanisha kwa tafsiri isiyo rasmo; "Maelezo ya kina kuhusu mtindo wa maisha ya Mobutu."

Mbali kuwa wake zao watatu, pia Mobutu alibahatika kuwa na watoto kadhaa kupitia kwa wanawake wengine ambao hawakuwa wake zake. Kuna mwanamke mwingine alijulikana kwa jina maarufu la "Mama 41,"puko wake, alizaa naye watoto watatu ambao ni Senghor, Dongo na Nzanga.

Mwanamke mwingine ambaye alipata naye mtoto alijulikana kwa jina la Mbanguula, pia alizaa naye kijana mmoja ambaye hafahamiki sana. Aidha, huko Brazzaville alizaa mtoto na mwanamke asiyejulikana sana, mtoto aliitwa Robert.

***Makala haya takayoendelea wiki ijayo imeandaliwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali mtandaoni.***



*Jana kamera ya Pambazuko imekuta Kituo cha Mabasi Yaendayo Haraka (Udart) cha Manzese, Dar es Salaam kikiwa kimeanza kufanyiwa ukarabati baada ya gazeti hili kuonyesha kituo hiki na vingine kutofanyiwa kwa wakati uliokuwa umeahidiwa na serikali baada ya vurugu za uchaguzi 2025.*

Na Anti MSHAURI





# Mtoto anahitaji muda wa mzazi

HABARI za leo msomaji wangu wa Safu ya Uhusiano karibu tuungane pamoja kujulishana masuala mbalimbali ya maisha.

Kwa siku zilizopita nimepokea ujumbe kutoka kwa wasomaji na baadhi ya maoni yakieleza baadhi ya wazazi kushindwa kutenga muda wa kukaa pamoja na watoto wao kwa mazungumzo na masuala yatokanayo na masomo na mambo mengine.

Amina Jumanne wa Dar es Salaam anasema “Baba wa watoto wangu anafanya kazi kwa saa 12, anarudi nyumbani, anakula, analala, wiki nzima hajui watoto wake wameishije nyumbani na shuleni; Pesa ipo, lakini upendo na ushauri haupo.”

Joseph Lambart, mkazi wa Arusha anasema enzi za ujana wake akiwa na wazazi aliishi nao na kupewa kila kitu, lakini wazaza hawakuwa na muda wa kukaa naye na kumuuliza changamoto na mengine mazuri na matokeo yake alitafuta upendo nje.

Mama Neema Jackson wa Mwanza anasema tatizo siyo kukosa muda, bali ni vipaumbele.

“Unakuta mzazi ana muda wa kuperuzi mitandaoni kama Tik Tok pengine kwa saa nzima, lakini anakosa dakika 10 za kukaa na mtoto wake na kusikia mazuri yake na changamoto anazopitia.

Maoni ya wasomaji hawa yanatafakarisha mengi. Suluhisho la haya yote ni kutenga muda maalum na watoto; chagua dakika 20 walau mara mbili au tatu kwa wiki. Hakuna simu, hakuna Televisheni, jitahidi kuuliza tu, leo(siku husika) kulikuwaje? Na na umsikilize vyema.

Lakini pia shiriki majukumu; baba na mama siyo kazi ya mtu mmoja; mmoja anafundisha hesabu, mwingine anasoma Biblia au hadithi na jingine jitahidini kuwa mfano kwa watoto.

Mtoto anajifunza kwa kukutazama kama wewe unakuwa umeshika simu wiki nzima na kuacha kuwa nao pamoja unamjenga kuiga ufanyayo.

Wazazi eleweni kuwa pesa italisha mtoto leo lakini muda wako ndio utamlea awe mtu wa kesho.

Tukutane wiki ijayo.

***Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0715 88 67 49.***

# Prisca Lyimo katika vazi la kipekee usiku wa Miss Cosmo

MWANAMITINDO na muigizaji, Prisca Lyimo, amevikwa rasmi taji la Miss Cosmo Tanzania 2026 kwenye usiku wa fainali kuu ya mashindano ya Miss Grand Tanzania na Miss Cosmo Tanzania.

Kama mshindi wa taji hilo, Prisca anajiandaa kuiwakilisha Tanzania kimataifa nchini Vietnam.

Muonekano wake uliyoandaliwa na chapa ya hapa nyumbani ya Neste Fashions, uliuteka uwanja na kuvutia macho ya watazamaji.

Gauni lake la kipekee limebuniwa na chapa mashuhuri ya mavazi nchini ya Neste Fashions.

Pia vazi lake hilo limetawaliwa na mchanganyiko wa rangi za kifahari za royal blue na purple zilizopambwa kwa ufundi wa juu wa mawe na shanga zinazong'aa.

Gauni hilo likiwa na mikono mirefu ya kitambaa chepesi huku shingo ikiwa ya wazi iliyoshuka chini na mpasuo mrefu unaoleta muonekano wa kisasa.

Mrembo huyo amenogesha muonekano wake na viatu virefu vya wazi pamoja na mtindo wa nywele fupi zilizowekwa vizuri upande mmoja.



## Fanya ngozi ya uso kuwa laini

NGOZI ya usoni inavutia kutokana na matunzo haswa kwa kufuata ratiba bora kuanzia namna ya kuosha hadi vitu unavyovitumia.

Hapa nimekuwekea vitu vingine vya kubusti mwonekano wako kama ifuatavyo;

Tumia mafuta ya vaseline ya mgando kijiko kimoja na kiini cha yai.

Osha vizuri uso wako kisha kausha vizuri.

Changanya mafuta na kiini cha yai koroga vyema na upake usoni kwa kujimasage, kaa na mchanganyiko usoni kwa dakika 30, kisha nawa kwa maji safi ya uvuguvugu usitumie sabuni.

Fanya hivi mara mbili kwa wiki na utaona matokeo.







# Lionel Richie 'awaponda' Usher, Chris Brown

Na Mwandishi WETU

MWANAMUZIKI mkongwe kutoka Marekani, Lionel Richie amewakosoa Usher Raymond na Chris Brown kuhusu ziara yao ya pamoja, akisema wasanii wawili wakubwa kushirikiana kwenye ziara siyo jambo jipya.

Mkongwe huyo akiwa jukwaani katika ziara yake na kundi la Earth, Wind&Fire, amesema wasanii hao wanaonekana kama wanajaribu kufanya jambo jipya, lakini yeye na wenzake walikuwa wakifanya aina ya ziara takriban miaka 40 iliyopita.

Richie akatoa utani uliowafanya mashabiki kucheka na kushangilia, akisema tofauti kubwa kati ya kizazi chao na cha Usher na Chris Brown ni kwamba wao "hawakwenda jela."

Kauli hiyo ilionekana kulenga hasa historia ya matatizo ya kisheria ya Chris Brown. Chris Brown amewahi kukabiliwa na kesi mbalimbali za kisheria, ikiwemo kesi maarufu ya mwaka 2009 iliyohusisha shambulio dhidi ya Rihanna.

Kwa hiyo, utani wa Richie ulitafsiriwa na wengi kama dongo la moja kwa moja kwa Brown, ingawa jina la Usher pia lilitajwa katika kauli hiyo.

# Mtoto wa Chameleon matatani Marekani

Na Mwandishi WETU

MTOTO wa mwanamuziki kutoka Uganda, Jose Chameleon, Abba Marcus Mayanja (20), ameripotiwa kukamatwa nchini Marekani na polisi akikabiliwa na tuhuma za shambulio dhidi ya mwanafamilia – lililofanyika nyumbani.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa na ukurasa wa Facebook wa Minneapolis Safety And Crime Alerts, Abba aliingizwa kwenye kumbukumbu za polisi Agosti 14, 2026, huku picha yake ikiambatana na maelezo ya tuhuma zinazomkabili.

Taarifa hiyo inadai kuwa Abba anachunguzwa kwa kosa la kiwango cha kumfanya mtu mwingine – akiwa ndani ya nyumba, ahofie kupata madhara ya haraka ya kimwili au kupoteza maisha. Kwa mujibu wa taarifa hiyo, hadi wakati wa kuchapishwa kwake Abba alikuwa bado anashikiliwa, huku dhamana yake ikitajwa kuwa dola 10,000 za Marekani (zaidi ya Shilingi milioni 27).



Abba Marcus ni mtoto wa kwanza wa Jose Chameleon, amekuwa akiishi na kusoma nchini Marekani.

# Simba atakula nyasi hadi lini?

Na John MARWA




WAHENGA walisema simba mwenda pole ndiye mla nyama, wakimaanisha kuwa mtu mpole siku zote ndiye mwenye mambo makubwa ama utuluvi, hivyo huleta ushindi mkubwa katika kila jambo.

Je, maneno ya wahenga yanapenya kwenye ngoma za masikio ya mashabiki wa Klabu ya Simba? Kwani ukimya wa Simba kwa misimu mitano mtawalia bila kunyanyua taji la Ligi Kuu Soka Tanzania Bara, unawatia shaka.

Wakati dirisha la usajili likifungwa, bado ndani ya Klabu ya Simba kunaonekana hakujakaa sawa katika baadhi ya maeneo kama kiungo wa ulinzi na eneo la ushambuliaji, jambo ambalo linaweka hofu kwa wahafidhina wa kandanda.

Licha ya kufanya usajili wa wachezaji watatu wa kigeni na wanne wazawa, bado roho za mashabiki "hazijawa kwatu" kutokana na kile ambacho wanakiona kwa watani wao; Yanga ambao wameanzia walipoishia msimu uliopita huku usajili wao ukitishia amani upande wa pili.

Ni kweli Simba wamekosa meno kabisa katika soko la usajili kutokana aina ya usajili ambao wamekuwa wakifanya hasa katika baadhi ya maeneo ndani ya klabu hiyo, huku nyota wengi wanaojiunga na timu hiyo wakiwa hawana viwango vinavyoridhisha mashabiki wao wengi.

Duru zinaeleza shida siyo pesa ndani ya klabu hiyo, bali ni namna mambo yanavyoendeshwa hasa katika meza ya utawala huku vita ya madaraka ikionekana kugawa klabu hiyo na kuisambaratisha dhana ya "Nguvu Moja" ambayo ndio kauli mbiu ya timu hiyo ya Msimbazi, Dar es Salaam.

Ni wazi kuna pande mbili hadi tatu ambazo kila moja inavutia kwake kutaka kuwa na nguvu ndani ya klabu. Hii ni ajabu kuona klabu yenye katiba lakini ikiendeshwa kwa kile kinachoweza kuelezwa kuwa ni ulaghai na kusababisha sintofahamu nyingi ndani ya kilabu hiyo.

Wapenzi wachache wa Simba sasa wameamua Mnyama huyo kula nyasi huku wakiwa wameshikilia vipande vya nyama mifukoni mwao.

Kutokana na hilo, hatma ya mafanikio kwa timu hiyo bado haieleweki kwa kuwa wapo waliofanikiwa azma yao – ya kuwagawa wana-Simba na kila mmoja analia na kulalama kwa harufu ya finyango za nyama wanazotupiwa.



# Utamu NBC PL warejea na FVS




**Na John MARWA**

UTAMU wa Ligi Kuu Soka Tanzania Bara umerejea wikiendi iliyopita kwa msimu wa NBC PL 2026/27 kuanza, kwa klabu 16 kumenyana katika michezo 30 dakika 2700.

Wakati mashabiki wakianza kufurahia ama kununa kwenye matokeo ya mechi, jambo kubwa lenye kuvutia msimu huu wa kandanda, ni Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kutambulisha teknolojia ya usaidizi wa mwamuzi ya 'Football Video Support' (FVS) ambayo ni mfumo mpya unaotumika sasa badala ya VAR.

FVS ina faida nyingi za kumsaidia mwamuzi kuwa na usahihi wa uamuzi na matukio yanayoweza kubadili mwelekeo wa mchezo ndani ya dakika 90 husika, ambayo inampa mwamuzi haki, uhakika na heshima bila kuharibu mtiririko wa mchezo.

Hizi ni faida tano kwa mwamuzi kutumia FVS; ni kupunguza makosa makubwa kama uhalali wa bao, pigo la mkwaju wa penati, kadi nyekundu ya moja kwa moja na kumtambua mchezaji. Pili husaidia kudhibiti kasi ya mchezo, FVS haiangalii kila kitu, bali mwamuzi ndiye anaomba tukio analohitaji kujiridhisha.

Pia, humsaidia mwamuzi kupunguza presha na kukosolewa kwani FVS ni ushahidi wa pili wa kuthibitisha uamuzi wake, hii hupunguza shinikizo la lawama na shutuma kwa waamuzi.

Faida nyingine ni kumsaidia mwamuzi kujifunza kutoka mchezo mmoja hadi mwingine kwa kuangalia upande ambao aliukosa katika tukio husika ili kuboresha uono wake katika matukio yatakayofanana na hilo kwa mechi zinazofuata.

Aidha, FVS hupatikana kwa gharama ndogo jambo ambalo kwa sasa hata ligi ndogo zinaweza kumpa mwamuzi msaada, hivyo teknolojia ya FVS ni msaada wa uamuzi kwa waamuzi wote kote ulimwenguni.

Hata hivyo, FVS hutumia kamera nne hadi sita na mtaalamu mmoja, wakati VAR huhitaji chumba cha VAR, kamera nane hadi 12 pamoja na zingine za mstari wa kuotea huku ikihitaji watu watatu hadi wanne.

Je, ni kwa kiasi gani FVS inaenda kupunguza lawama ambazo zimekuwa zikitupwa kwa waamuzi kwa kushindwa kutoa tafsiri sahihi za sheria za soka na faida kwa timu isiyostahili, ni jambo la kusubiri kuona vile kutaenda kwa msimu mzima.

*GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.*

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS ASSOCIATION